**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

---

# WIZARA YA AFYA ZANZIBAR

**HOTUBA YA KAIMU WAZIRI WA AFYA**

**MHE DKT. SAADA MKUYA SALUM**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI**

**YA WIZARA YA FYA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

***Mei, 2026***

## YALIYOMO

*Mada* *Ukurasa*

**MCHANGANUO WA VIFUPISHO** .......... **iii**

**A. UTANGULIZI** .......... **1**

B. **MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA** .......... 7

**C. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26** .......... **9**

**D. MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** .......... **11**

**E. MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA AFYA** .......... **12**

**F. PROGRAMU KUU: KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)** .......... *14*

- o ***Huduma za Mapambano dhidi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma*** .......... ***16***
- *o* ***Huduma za kumaliza Malaria Zanzibar*** .......... ***19***
- *o* ***Kuimarisha huduma za Lishe, afya ya Uzazi, Mama na Mtoto*** .......... *20*
- *o* ***Huduma ya Maradhi Yasiyoambukiza*** .......... ***23***
- *o* ***Huduma za Ufuatiliaji na Uratibu wa Maradhi ya Miripuko na Dharura za Kiafya*** .......... ***24***
- ***o*** ***Huduma za maradhi yasiyopewa kipaumbele*** .......... ***24***
- ***o*** ***Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho*** .......... ***24***
- ***o*** ***Huduma za Elimu ya Afya*** .......... ***27***
- ***o*** ***Huduma za Uratibu wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (CHW)*** ... *28*
- *o* ***Huduma ya Afya ya Mazingira*** .......... ***28***
- *o* ***Huduma za Afya ya Mipakani (Bandarini na Viwanja vya ndege)*** ...... ***30***
- *o* ***Huduma za Afya ya Wafanyakazi*** .......... ***31***
- *o* ***Huduma za Afya ya Msingi ya Akili*** .......... ***32***
- *o* ***Huduma za Damu Salama*** .......... ***32***
- *o* ***Huduma za Maabara ya Afya ya Jamii*** .......... ***32***

**G. PROGRAMU KUU: HUDUMA ZA TIBA (PH0102)** .......... **33**

**H. PROGRAM NDOGO: HUDUMA ZA MATIBABU (SH010201)** .......... *35*

- o ***Huduma za Uchunguzi wa Maradhi*** .......... ***36***
- *o* ***Huduma za Matibabu*** .......... ***37***
- *o* ***Huduma za Ushirikiano wa Afya Kimataifa*** .......... ***37***
- *o* ***Huduma ya Mkono Kwa Mkono (One Stop Centre)*** .......... ***39***
- *o* ***Huduma za Bodi na Mabaraza ya Taaluma za Afya*** .......... ***40***
- *o* ***Baraza la Madaktari*** .......... ***40***
- *o* ***Baraza la Wataalamu wa Maabara za Tiba*** .......... ***40***
- *o* ***Baraza la Wauguzi na Ukunga*** .......... ***41***
- *o* ***Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi*** .......... ***41***
- *o* ***Baraza la Taaluma za Afya ya Jamii na Mazingira*** .......... 42
- *o* ***Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala*** .......... 42

*Mada* *Ukurasa*

- *o* ***Huduma za Uuguzi na Ukunga*** ... ***43***
- *o* ***Huduma ya Upatikanaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi*** ... ***44***
- *o* ***Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa*** ... **44**

**I. PROGRAM NDOGO: HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH010202)** ... *46*
- *o* ***Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi*** ... ***46***
- *o* ***Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali*** ... **48**

**J. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PH0103) 50**

**K. PROGRAMU NDOGO: UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301)** ... ***52***
- *o* ***Kuimarisha Nguvukazi kwa Sekta ya Afya*** ... ***52***
- *o* ***Uratibu wa Manunuzi, Fedha na Ukaguzi wa Wizara*** ... ***53***
- *o* ***Mifumo ya Digitali na Taarifa za Afya*** ... 54

**L. PROGRAMU NDOGO: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302)** ... 55
- o **TAASISI YA UTAFITI WA AFYA (ZAHRI)** ... 59

**M. PROGRAM NDOGO: URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA AFYA PEMBA (SH010303)** ... **60**

**N. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA AFYA** ... **61**

**O. PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)** ... **68**

**P. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ... **70**

**Q. HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO** ... **71**

**R. MUELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27** ... **72**

**S. MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27** ... *75*

**T. MAELEZO YA BAJETI KWA PROGRAMU** ... **76**
- **i. PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA** ... **76**
- **ii. PROGRAMU YA TIBA** ... **76**
- **iii. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PHO103)** ... 76
- **iv. PROGRAMU ZA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA FUNGU (025)** ... **77**

**U. SHUKURANI** ... **77**

**V. HITIMISHO** ... ***79***

**MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA KAZI ZILLIZOPANGWA KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** ... **79**
- o ***Mapato*** ... ***81***
- *o* ***Matumizi*** ... 81

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ARV | - | Anti-Retroviral Virus |
| BADEA | - | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| BOQ | - | Bill of Quantities |
| CBM | - | Christian Blind Mission |
| CDC | - | Centre for Disease Control and Prevention |
| CHW | - | Community Health Workers |
| CT Scan | - | Computed Tomography |
| ECSA-HC | - | The East, Central and Southern Africa Health Community |
| eLMIS | - | Electronic Logistic Management Information System |
| EMR | - | Electronic Medical Records |
| GIZ | - | German Agency for International Cooperation |
| HIPZ | - | Health Improvement Project Zanzibar |
| HPV2 | - | Human papillomavirus types 2 (HPV-2) |
| IPC | - | Infection Prevention Control |
| JKCI | - | Jakaya Kikwete Cardiac Institute |
| KCMC | - | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| MOI | - | Muhimbili Orthopaedic Institute (MOI) |

| | | |
|---|---|---|
| MRI | - | Magnetic Resonance Imaging |
| PDB | - | Presidential Delivery Bureau |
| PENTA 3 | - | Pentavalent vaccine 3 |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNFPA | - | United Nations Population Fund |
| UNICEF | - | United Nations Children’s Fund |
| VVU | - | Virusi Vya UKIMWI |
| WHO | - | World Health Organization |
| ZAHRI | - | Zanzibar Health Research Institute |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naanza Hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kuhudhuria katika kikao cha kujadili Hotuba ya makadirio na mapato ya Wizara ya Afya. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uwezo, nguvu na busara za kutekeleza majukumu tuliyojipangia.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nachukuwa fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuchaguliwa kwa awamu ya pili kupitia uchaguzi ulifanyika mwezi Octoba 2025 ushindi huo ni ishara kuwa wananchi wanaimanani na Mheshimiwa Raisi na Serikali anayoingoza. Aidha, namshukuru kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kutoa miongozo, maelekezo na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta hii muhimu kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Kwa kupitia miongozo, maelekezo na ushirikiano wake anaotupatia umerahisisha kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa **Hemed Suleiman Abdullah, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar** kwa mashirikiano mazuri anayompatia Mheshimiwa Rais katika kuingoza nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile nachukuwa fursa hii kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuchaguliwa kuingoza Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. **Mheshimiwa Spika;** Napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili kwa umakini kabisa pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa baraza na Kamati za Kudumu ikiwemo Kamati ya Ustawi wa Jamii, kamati ya Bajeti na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna wanavyotoa hoja na michango ili kuleta ufanisi na uwajibikaji wa watendaji wa taasisi mbali mbali.

5. **Mheshimiwa Spika**, Kwa unyenyekevu na Moyo wa shukurani napenda kutoa pongezi za dhati kwa wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya wakiwemo, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu, Afisa Mdhamini Wizara ya Afya Pemba, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Divisheni na Vitengo vilivyo chini ya Wizara ya Afya. Aidha, kwa dhati kabisa nawashukuru wenyeviti na wajumbe wa Bodi za ushauri za Taasisi na Mabaraza ya Wataalamu yaliyochini ya Wizara ya Afya kwa michango, ushauri, busara, hekima, miongozo na mashirikiano makubwa wanayotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.Pia nawashukuru watendaji wengine wote wa Wizara ya Afya kuanzia ngazi ya jamii, Vituo vya Afya, Hospitali, Programu

na Vitengo vyote kwa kujituma kwa moyo katika kuwahudumia wananchi. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa imani na uzalendo kwa nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/ 2027 ikijumuisha Mafanikio, Muundo na Majukumu ya Wizara, Utekelezaji wa Programu kuu, Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/2026, Changamoto zilizojitokeza na utatuzi. Aidha, ***Mheshimiwa Spika, naomba hotuba hii iingie katika kumbukumbu ya Baraza lako tukufu pamoja na muhtasari huu, kama ilivyo katika kitabu kilichowasilishwa.***

7. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya kutoa maelezo yangu ya awali, naomba sasa kutambua mafanikio ya sekta ya afya kwa kipindi 2025/2026 yaliyotokana na uwekezaji mkubwa uliowekwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika sekta ya afya kama ifuatavyo: -

## 1.0 UONGOZI NA USIMAMIZI WA SEKTA YA AFYA

Katika Kipindi cha Utekelezaji 2025/2026 wizara imepata mafanikio yafuatayo: -

i. Kufanya mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2011 na kuandaa rasimu ya Sera ya Afya ya mwaka 2026;
ii. Kuandaa miongozo ya Rufaa; na
iii. Kuanzishwa Idara ya Ufundi na Miundo mbinu ya Afya.

## 2.0 MIUNDOMBINU YA AFYA

Katika uimarishaji wa miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma, Wizara ya afya imeweza kuimarisha yafuatayo**: -**

i. Kukamilika na kutumika kwa nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali ya Kitogani, Mwerapongwe, Pangatupu kwa upande wa Unguja na Hospitali Kinyasini kwa upande Pemba;

ii. Kukamilika kwa ujenzi, kufunga vifaa tiba na kuanza utoaji wa huduma kwenye Hospitali ya wagonjwa wa Afya ya Akili Pandani Pemba na Kituo cha Afya Kinduni Unguja;

iii. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya afya ambapo vituo vya Afya (Health Centers) **6** (Magomeni wandaras, Sebleni, Tunguu na Tumbatu kwa Unguja na Jadida kwa Pemba);

iv. Kuanza kwa mradi wa ujenzi Hospitali za Mkoa wa Kaskazini Mahonda na Vituo vya Afya ikiwemo vituo vya Afya (Health Centers) **10 (**Kojani, Welezo, Mtoni Basra, Maziwa ng'ombe, Fuoni na Jang'ombe);

v. Kuongezeka kwa gari za kubebea wagonjwa (ambulance) kutoka **26** kwa mwaka 2024 kufikia **46** kwa mwaka 2026;

vi. Kuanza kwa ujenzi wa Taasisi ya Umahiri wa Matibabu ya Saratani Zanzibar (Zanzibar Cancer Institute);

vii. Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi katika mwaka wa Fedha 2025/2026 hali ya upatikanaji wa dawa na Vifaa tiba kwa ngazi ya Vituo vya Afya ya Msingi wamefikia asilimia **83.7** kutoka asilimia **80** kwa Fedha 2024/2025.

Aidha, Katika Hospitali za Wilaya na Mikoa upatikanaji wa Dawa umengezeka kutoka asilimia **95** ya malengo na kufikia asilimia **97**.

## 3.0 NGUVU KAZI KATIKA SEKTA YA AFYA

i. Wafanyakazi **237** wamepelekwa masomoni wakiwemo (madaktari bingwa Bobezi 4); Wabobezi Macho wa watoto **2** (Paediatric Opthalmologist), Ganzi na Usingizi wa Watoto **1**(Paediatric Anaesthesiologist) na Daktari bingwa bobezi wa watoto wachanga **1**(Neonatologist);

ii. Jumla ya watumishi 116 wamerudi masomoni wakiwemo Daktari Bingwa wa kinamama 2, Daktari Bingwa wa Watoto 3, Dakatri wa Women Images 1, na kada nyengine kama inavyoonekana katika **kiambatisho 5b;**

iii. Kuanzishwa kwa Mfumo wa Rasilimali watu wa Afya (ZanHRH) ambapo kwa sasa unatumika Rasmin kwa lengo la kuboresha upatikani wa Taarifa za watumishi;

iv. Kupatikana kwa Mpango wa Rasilimali watu na Muongozo wa Mafunzo endelevu kwa kada za Afya ili kutekeleza majukumu ya Wafanyakazi wa Afya kwa ufanisi (Continuous Professional Development).

## 4.0 UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA

Kwa upande wa utoaji wa huduma mafanikio yaliopatikana ni: -

i. Kukamilika na kuanza kwa huduma za Kibingwa za Uchunguzi na Matibabu ya uzibuaji wa Mishipa ya moyo

(Cath lab), Upasuaji wa matundu madogo kwa kutumia kamera (Laparascopic Surgery) katika Hospitali ya Lumumba;

ii. Kuendelea kwa mashirikiano ya utoaji wa huduma bora za kibingwa na bobezi kwa kushirikiana na Taasisi na Wataalamu kutoka nje na ndani ya Tanzania ikiwemo Hospitali ya Benjamin Mkapa (Matibabu ya Figo na Upandikizaji wa Uroto) upandikizaji nyonga na magoti bandia, matibabu ya Ubongo na mishipa ya fahamu, Moyo (kuweka Pace Maker) nk.;

iii. Kupungua kwa vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi kutoka vifo **145** kwa mwaka 2023 hadi kufikia vifo **121** kwa mwaka 2025; kwa kila vizazi hai **100,000**.

## 5.0 KUGHARAMIA HUDUMA ZA AFYA

i. Kuanzisha Mfuko maalum wa maendeleo ya Afya Zanzibar (Health Development Fund);

ii. Ongezeko la Bajeti katika sekta ya afya kutoka **368.15 bilioni** kwa mwaka 2025/2026 hadi kufikia **405.89 bilioni** kwa mwaka 2026/2027 sawa na ongezeko la asilimia **10.3.**

## 6.0 TAARIFA ZA AFYA NA MIFUMO YA TEHAMA

Wizara imefanikiwa kuimarisha mifumo ya taarifa za afya kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha miundombinu ya **TEHAMA** na matumizi ya mfumo wa ZanEMR kwenye Vituo vya Afya Ngazi ya Msingi;

ii. Kupunguza Mifumo na kuweza kusomana (interoperability) kutoka **43** hadi **23.**

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA

8. **Mheshimiwa Spika**, Wizara hii inaundwa na Idara sita (**6**) na Ofisi kuu Pemba, Taasisi tano (**5**), Bodi na Mabaraza saba (**7**) ya taaluma mbalimbali za kiafya zinazolinda maadili na kusimamia taaluma za afya. Dhamira ya Wizara ya Afya ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zinazotolewa katika hali ya ubora, usawa na ufanisi kwa watu wote wa Zanzibar. Wizara ya afya ina majukumu yafuatayo: -

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara;
ii. Kushajihisha kufanya tafiti za Afya kwa kupelekea maendeleo ya Sekta na Afya ya Jamii;
iii. Kuhamasisha upatikanaji endelevu wa rasilimali fedha utakaowezesha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote;
iv. Kusimamia utoaji wa huduma za Afya;
v. Kuhakikisha upatikanaji wa viwango bora vya huduma ya Afya katika ngazi zote kwa kuwafikia wananchi wote ikiwemo afya ya mama, mtoto, vijana na lishe;
vi. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza, magonjwa yanayoathiri Afya ya Akili, athari za ajali na afya mazingira kudhibiti maambukizi mapya ikiwemo maradhi ya miripuko;
vii. Kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma za uchunguzi wa maradhi, matibabu, utengamao na shufaa, na utoaji wa rufaa katika ngazi zote za kutolea huduma ya afya;

viii. Kusimamia huduma za tiba asili na tiba mbadala zilizo bora na salama nchini;

ix. Kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya ikiwemo majengo, mtandao wa teknolojia ya mawasiliano, vifaa tiba na usafiri;

x. Kuimarisha upatikanaji, uhifadhi, usambazaji na matumizi sahihi ya dawa, vifaa tiba, vitendanishi na miongozo ya matibabu katika ngazi zote za huduma ya afya;

xi. Kuhakikisha usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba;

xii. Kuhakikisha vifaa, vifaa tiba na miundombinu bora ya utoaji wa huduma;

xiii. Upatikanaji wa madaktari bingwa na wataalam wengine katika ngazi zote ikiwemo kuongeza na kuendeleza wataalamu wa afya wenye ujuzi, uwezo na maadili;

xiv. Kusimamia na kushajihisha elimu ya Afya kwa Jamii dhidi ya kinga ya maradhi mbalimbali ya kuambukiza na yasio ambukiza;

xv. Kuimarisha ubora na matumizi ya taarifa za afya katika kufanya maamuzi sahihi; na

xvi. Kuimarisha huduma za maabara za uchunguzi wa ubora na usalama wa vyakula, dawa, kemikali, maji, maji taka, sampuli za kijinai, sumu, vinasaba, udhibiti wa kemikali na tafiti.

## C. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

**9. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021/2022 – 2025/2026), Sera ya Afya ya Mwaka 2011 ambayo imeshafanyiwa mapitio mwaka 2026, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025, Mpango Mkakati wa tano wa Sekta ya Afya - (HSSP V 2026 – 2030), Maagizo na Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Sekta ya Afya pamoja na makubaliano ya Kikanda na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

**10. Mheshimiwa Spika,** Katika bajeti ya mwaka 2025/2026, Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali na Washirika wa Maendeleo ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya ikiwemo matengenezo ya majengo na vyombo vya usafiri;

ii. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na vitendanishi katika vituo vya afya ngazi ya msingi na Hospitali;

iii. Kuimarisha mifumo ya kidigitali ya taarifa za afya katika vituo vya afya ngazi ya msingi na Hospitali;

iv. Kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa na kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

v. Kuimarisha mifumo endelevu ya kugharamia huduma za afya ikiwemo Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar;

vi. Kuimarisha huduma za afya ya msingi kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii;

vii. Kupunguza vifo vya mama wajawazito kutoka vifo **145** kwa mwaka 2023 kwa kila vizazi hai **100,000** dhidi ya lengo la vifo **123** kwa kila vizazi hai **100,000** (Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050) na kufika vifo **70** kwa kila vizazi hai **100,000** (SDG-2030) ifikapo 2030;

viii. Kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo **28** kwa kila vizazi hai **1,000 (2019)** na kufikia vifo **26** kwa kila vizazi hai **1,000** (Dira ya Maendeleo ya Zanzibar **2050**) hadi kufikia vifo **12** kwa kila vizazi hai **1,000** (SDG- 2030) ifikapo mwaka 2030;

iv. Kuimarisha uwezo na utayari wa kukabiliana na majanga ya mripuko na matukio mengine ya kiafya;

x. Kuendeleza mapambano ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza; na

xi. Kuongeza idadi ya tafiti za afya kwa kuzingatia ajenda za nchi na kufanya uchambuzi wa tafiti hizo kwa lengo kutunga sera na miongozo ili kuimarisha huduma.

**10. Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kupitia program kuu **5** Fungu **H01 (3)** na Fungu **H02 (2):**-

i. Programu ya Kinga na Elimu ya Afya;

ii. Programu ya Huduma za Tiba;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara;

iv. Programu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu; na

v. Programu ya Uongozi na Utawala wa Hospitali.

## D. MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### MAPATO

**11. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara imekadiriwa kukusanya **TZS 6.97 bilioni** kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Wizara ilikadiriwa kukusanya **TZS 5.22 bilioni** ambapo hadi kufikia Machi 2026, Jumla ya **TZS 4.89 bilioni** zimekusanywa sawa na asilimia **94** ya makadirio. **(Kiambatisho 1(a) kinafafanua zaidi).**

### MATUMIZI

**12. Mheshimiwa Spika,** Programu hizo zote zilitekelezwa kwa mashirikiano makubwa kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo pamoja na jamii kwa ujumla. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 **TZS 368.15 bilioni** zilitengwa kupitia fungu **(H01)** ambapo **TZS 82.68 bilioni** kwa ajili ya

mishahara, **TZS 85.02 bilioni** kwa Matumizi Mengineyo, **TZS 188.24 bilioni** kwa miradi ya maendeleo na **TZS 12.21 bilioni** ni Ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara.

13. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 185.42 bilioni** sawa na asilimia **67** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 58.79 bilioni** sawa na asilimia **95** ya makadirio ya miezi tisa zilitumika kwa Mishahara na **TZS 66.93 bilioni** sawa na asilimia **105** ya makadirio ya miezi tisa zimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 53.19 bilioni** sawa na asilimia **38** ya makadirio ya miezi tisa zilitumika kwa Miradi ya Maendeleo na **TZS 6.51 bilioni** sawa na asilimia **71** ya makadirio ya miezi tisa zimetumika kwa Ruzuku za Taasisi zilizo chini ya Wizara. **(Kiambatisho 1(b) kinafafanua zaidi).**

## E. MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA AFYA

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, **TZS 188.24 bilioni** zilitengwa kutekeleza miradi ya maendeleo, kati ya hizo **TZS 83.45 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 104.79 bilioni** kutoka Washirika wa Maendeleo (**TZS 53.93 bilioni** ni msaada na **TZS 50.86 bilioni** ni mkopo).

15. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 53.19 bilioni** sawa na asilimia **38** zimetumika, kati ya hizo **TZS 31.56 bilioni** sawa na asilimia **38** kutoka Serikalini na **TZS 21.63 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS 18.02 bilioni** msaada na **TZS 3.61 bilioni** mkopo).

16. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipanga kutekeleza miradi ya maendeleo ifuatayo: -

i. Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi;

ii. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mkoa;

iii. Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya **(Kiambatisho 1(d) kinafafanua zaidi).**

iv. Kuimarisha mifumo ya kidijitali;

v. Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto;

vi. Programu Shirikishi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma;

vii. Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar;

viii. Programu ya Jamii ni Afya;

ix. Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar;

x. Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja;

xi. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia – Binguni; na

xii. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Saratani- Binguni.

## F. PROGRAMU KUU: KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)

17. **Mheshimiwa Spika,** Progaramu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kinga na kuongeza uelewa wa jamii juu ya njia mbalimbali za kujikinga na maradhi yakiwemo ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **TZS 103.98 bilioni** kati ya hizo **TZS 24.65 bilioni** kwa ajili ya mishahara, **TZS 10.93 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 68.40 bilioni** (**TZS 27.00 bilioni** kutoka Serikalini, **TZS 41.40 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS 16.40 bilioni** ni msaada na **TZS 25.00 bilioni** mkopo) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

19. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 52.15 bilioni** sawa na asilimia **67** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 18.75 bilioni** Mishahara na **TZS 2.13 bilioni** Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **TZS 31.27 bilioni** zilipatikana (**TZS 13.27 bilioni** kutoka Serikalini, **TZS 18.00 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS 14.56 bilioni** Msaada na **TZS 3.44 bilioni** Mkopo).

Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo: **-**

i. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutoa huduma za ushauri nasaha, upimaji na matibabu;

ii. Kuendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini;

iii. Kuimarisha huduma za lishe, afya ya uzazi, mama na mtoto;

iv. Kuimarisha huduma za afya ya Mipakani (Bandarini na Viwanja vya ndege);

v. Kuendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa maradhi ya macho katika vituo vya afya, hospitali, skuli na jamii;

vi. Kuendelea na mikakati ya kupambana na maradhi yanayoambukiza, yasiyoambukiza na kutokomeza maradhi yasiyopewa kipaumbele;

vii. Kuimarisha huduma za msingi za afya ya akili;

viii. Kuimarisha afya ya jamii na mazingira;

ix. Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali zitakazotoa matokeo ili kuimarisha huduma za afya katika kupambana na maradhi;

x. Kuimarisha huduma za afya ya msingi kwa kuwatumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii;

xi. Kuimarisha programu za uhamasishaji na kutoa elimu ya afya katika ngazi zote;

xii. Kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya; na

xiii. Kuongeza ukusanyaji wa damu.

**Huduma za Mapambano dhidi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma**

**20. Mheshimiwa Spika,** Wateja (Clients) **129,741** (Wanaume **57,615** na Wanawake **72,126**) walipatiwa huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa VVU, kati ya hao **827** (Wanaume **289** na Wanawake **538**) waligundulika na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **0.6**. Aidha, wateja wapya **892** walisajiliwa kwenye Vituo vya Huduma na Tiba kwa Watu Wanaoishi na VVU (CTCs) ambapo (Wanaume **269**, Wanawake **623** na Watoto **17**). **Kiambatisho Nambari 2a kinafafanua.**

**21. Mheshimiwa Spika,** Katika kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, wajawazito **55,345** walihudhuria kliniki wakati wa ujauzito. Kati ya hao, wajawazito **52,556** sawa na asilimia **95** waliopimwa na kujua hali zao za VVU ambapo **84** sawa na asilimia **0.2** waliogundulika na VVU. Kwa upande wa watoto wachanga **367** walipimwa kipimo cha DNA-PCR ndani ya miezi miwili ambapo maambukizi yaligundulika kwa mtoto **1** ikilinganishwa na watoto **351** waliopimwa mwaka 2024/2025 ambapo watoto **5** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU.

**22. Mheshimiwa Spika,** Wateja **10,252** (Wanawake **7,181** na Wanaume **3,071**) wanaendelea kupata huduma za VVU katika Vituo vya Huduma na Tiba (CTCs) Unguja na Pemba.

Hadi kufikia Machi 2026, wateja **9,817** (wanaume **2,938** na wanawake **6,879**) sawa na asilimia 95.7 wanatumia dawa za kupunguza makali ya virusi vya Ukimwi (ARV). hali hii inaonesha kuwa tumefikia maelengo ya ulimwengu ya kuhakikisha kuwa asilimia 95 yawaliopata maambukizi wapo kwenye matibabu ya kupunguza maambukizi ya VVU.

23. **Mheshimiwa Spika,** Wagonjwa **25,170** (Wanaume **5,404** na Wanawake **19,766**) wamegundulika kuwa na dalili na ishara na maradhi ya kujamiiana katika vituo vya afya na hospitali. Idadi hii imeongezeka ikilinganishwa na wagonjwa **22,493** (wanaume **4,522** na wanawake **17,971**) waliogundulika kwa mwaka 2024/2025. **Kiambatisho Nambari 2b kinafafanua.**

24. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma zinaendelea kutolewa katika hospitali na vituo vya afya ambapo wagonjwa **808** (Unguja **664** na Pemba **224**) waligundulika na Kifua Kikuu na wote walianzishiwa matibabu. Aidha, wagonjwa **66** waligundulika kuwa na maambukizi ya Kifua kikuu na VVU kwa pamoja (HIV/TB Co-infection) na wagonjwa **3** waligundulika kuwa na kifua kikuu sugu kati ya hao wanaume **2** na mwanamke **1**. Vile vile, wagonjwa wapya wa ukoma **53** (Unguja **45** na Pemba **8**) kati ya hao, wanaume **38** na wanawake **15** waligundulika ikilinganishwa na wagonjwa **60** (Unguja **52** na Pemba **8**) kwa mwaka 2025/2026.

25. **Mheshimiwa Spika,** Wateja **1,838** (Wanaume **1,752** na Wanawake **86**) wamendelea kutumia dawa kwenye Kituo cha Huduma ya Uraibu *(Methadone Assisted Therapy Clinic)* katika Hospitali ya Kidongo Chekundu Unguja. Aidha, kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, wateja wapya **11** wamesajiliwa na kujiunga na huduma.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuimarisha Huduma ya Homa Ini ambapo, wateja **28,735** (Wanaume **18,979** na Wanawake **9,756**) walipimwa ugonjwa wa Homa ya Ini **B**, kati yao wateja **439** waligundulika na maambukizi. Kwa upande wa Homa ya Ini **C**, Wateja **29,292** (Wanaume **18,292** na Wanawake **8,000**) walipimwa na **121** (Wanaume **100** na Wanawake **21**) waligundulika na ugonjwa huo. Huduma za uchunguzi zimepungua ikilinganishwa na mwaka 2024/2025 ambapo watu **30,412** walichunguzwa na kugundulika na maambukizo ya Homa ya Ini **B** na watu **27,926** Homa ya Ini **C**. Hii ilitokana na kupungua kwa Huduma ya Mkoba (Outreach) katika ngazi ya Jamii. Wizara itahakikisha inaimarisha huduma za mkoba ili kuongeza uchunguzi katika ngazi ya jamii. **Kiambatisho Nambari 2c (1) kinafafanua.**

27. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, wagonjwa wa Homa ya Ini **B**, **4,155** (Unguja **3,383** na Pemba **772**) wamesajiliwa katika kliniki zinazotoa huduma za tiba ya Homa ya Ini **B**. Aidha, wagonjwa **407** (Unguja **369** na

Pemba **38**) wa Homa ya Ini **C** wamesajiliwa katika kliniki za huduma na tiba. Vile vile, wagonjwa **316** wanaendelea kupata matibabu ya ugonjwa Homa ya Ini **B** na wagonjwa **97** wanaendelea kupata matibabu ya Homa ya Ini **C**. **Kiambatisho Nambari 2c (2, 3) kinafafanua.**

**Huduma za kumaliza Malaria Zanzibar**

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kumaliza Malaria Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, washukiwa **492,513 (**Unguja **394,014** na **98,499** Pemba**)** wamechunguzwa vimelea vya malaria ambapo **7,654 (**Unguja **7,190,** na Pemba **484)** sawa na asilimia **1.6** wamegundulika kuwa na vimelea vya malaria.

**29.** **Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,** Katika juhudi za kudhibiti mbu waenezao Malaria, zoezi la upigaji dawa majumbani limefanyika katika Wilaya **8** (Unguja **5** na Pemba **3**). Nyumba **3,564** (Unguja **2,436** na Pemba **1,128**) zimepigwa dawa ya kuuwa mbu waenezao malaria. Aidha, vyandarua **16,841** vyenye dawa ya muda mrefu vimetolewa katika wilaya zote kupitia kliniki ya mama na mtoto katika vituo vya afya. Afua hizo zimesaidia kupunguza visa vya malaria kutoka **22,102** (2024/2025) hadi kufikia **17,118** (2025/2026).

**Kuimarisha Huduma za Lishe, Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto;**

30. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026**,** Mama wajawazito **56,774** (Unguja **42,007** na Pemba **14,767**) walihudhuria katika kliniki na kupatiwa huduma za upimaji. Aidha, wajawazito **42,697** wamejifungua, kati ya hao wajawazito **36,369** wamejifungua kwa njia ya kawaida na wajawazito **6,328** wamejifungua kwa njia ya upasuaji katika vituo vya afya na hospitali na wajawazito **1,779** wamejifungua nyumbani. Wajawazito wote hao wamepatiwa huduma ndani masaa **48** baada ya kujifungua. Takwimu zinaonyesha kupungua kwa wajawazito kujifungualia nyumbani ikilinganishwa na mwaka 2024/2025 ambapo wajawazito **1,957** wamejifungua nyumbani. Aidha, takwimu zinaonyesha idadi ya mama wanaojifungua vizazi hai katika hospitali na vituo vya afya imeongezeka kutoka **53,529** kwa mwaka 2024 hadi kufikia **62,201** kwa mwaka 2025. **Kiambatisho Nambari 3a kinafafanua**.

31. **Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kuekeza katika eneo la huduma za mama na mtoto na kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua mbalimbali zilizopelekea kupungua vifo vya mama vinavotokana na ujauzito kutoka vifo **145** kwa kila vizazi hai **100,000** kwa mwaka 2023 hadi vifo **121** kwa kila vizazi hai **100,000** kwa mwaka 2025. Aidha, kwa upande wa vifo

vya watoto wachanga ndani ya mwezi mmoja baada ya kuzaliwa vimepungua kutoka vifo **13.2** katika kila vizazi hai **1,000** kwa mwaka 2023 hadi kufika **11** katika kila vizazi hai **1,000** kwa mwaka 2025 (DHIS2). Hali hii ya kupungua kwa vifo vya mama na watoto inaonesha kuwa tupo kwenye muelekeo mzuri ya kuyafikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 pamoja na Malengo Endelevu ya Dunia (SDG-2030). **Kiambatisho Nambari 3b kinafafanua**

**32. Mheshimiwa Spika,** Katika kupunguza vifo vya mama na watoto wachanga, wizara inaendelea kutekeleza mfumo wa huduma za rufaa kwa mama wajawazito na watoto wachanga (M-mama). Mama **959** (**546** Unguja na **413** Pemba) na watoto wachanga **128** (**110** Unguja na **18** Pemba), walipatiwa huduma ya rufaa. Idadi hii imeongezeka ikilinganishwa na akinamama **724** na watoto wachanga **69** waliopatiwa rufaa mwaka 2024/2025.

**33. Mheshimiwa Spika,** Wateja wapya **23,491** (Unguja **18,162** na Pemba **5,329**) walijiunga na njia mbalimbali za uzazi wa mpango. Idadi hii inaonesha kupungua ikilinganishwa na takwimu ya mwaka 2024/2025 ambapo wateja wapya walikua **27,440** (Unguja **19,240** na Pemba **6,845**). Uhamasishaji wa uzazi wa mpango unaendelea kwa wakinababa na mama ili kuhakikisha mila na desturi zinabadilika na kuengeza idadi ya wateja wapya na kuimarisha afya ya uzazi kwa mama na mtoto.

34. **Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na mkakati wa kuwakinga watoto na magonjwa hatarishi, ambapo watoto **74,416** (Unguja **53,777** na Pemba **20,639**) wamepatiwa dozi ya BCG, Watoto **51,253** (Unguja **33,481** na Pemba **17,772**) wamepatiwa dozi ya tatu ya POLIO (OPV3) na Watoto **50,993** (Unguja **33,192** na Pemba **17,801**) wamepatiwa dozi ya tatu ya PENTA. Kwa upande wa chanjo ya surua (MR2) watoto **57,298** (Unguja **40,138** na Pemba **17,160**) walipatiwa chanjo hiyo. Aidha, wasichana **17,610** (Unguja **11,695** na Pemba **5,915**) walipatiwa dozi ya chanjo ya kukinga saratani ya shingo ya kizazi (HPV2) ikilinganishwa na wasichana **10,696** waliopatiwa chanjo hio mwaka 2024/2025. **Kiambatisho Nambari 3c kinafafanua zaidi**.

35. **Mheshimiwa Spika,** Watoto **236,672** (Unguja **153,611** na Pemba **83,061**) wenye umri wa miezi **6-59** wamepatiwa virutubisho vya vitamini **A** sawa na asilimia **91** ya waliotarajiwa ambapo huduma hiyo ilipangwa kutolewa kwa watoto **260,917** ambapo idadi hii imeshuka ikilinganishwa na mwaka 2024/2025 ambapo asilimia **94** ya watoto walipatiwa virutubisho.

36. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha hali ya lishe watoto **170** (Unguja **118** na Pemba **52**) walifikiwa na kupatiwa huduma za matibabu ya utapiamlo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano **(5)** pamoja na kuwapa elimu walezi wao kwa kutumia jiko darasa katika Wilaya nne; Unguja (Kaskazini A, Kaskazini B) na Pemba (Wete na

Micheweni). Mikakati hiyo imesaidia kupunguza asilimia ya watoto wenye uzito pungufu kulingana na umri kutoka asilimia **5.5** (2024/2025) hadi asilimia **3.5** (2025/2026). Aidha, asilimia ya watoto wenye udumavu kulingana na umri na urefu imepungua kutoka asilimia **3.9** (2024/2025) hadi asilimia **3.4** (2025/2026)

**Huduma ya Maradhi Yasiyoambukiza;**

**37. Mheshimiwa Spika,** Katika kudhibiti na kupunguza maradhi yasioambukiza, watu **189,964** (wanaume **56,319** na wanawake **133,645**) walifanyiwa uchunguzi katika jamii na Vituo vya Afya vinavyotoa huduma za maradhi yasioambukiza. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonyesha kuwa wagonjwa wapya wa kisukari walikuwa **5,697 (3%)**, **72,186 (38%)** walikuwa na uzito uliozidi na **5,699 (3%)** walikuwa na uzito hafifu. Aidha, watu **18,996 (10%)** walibainika na visa vipya vya shinikizo la juu la damu na wagonjwa **324** wa saratani wameripotiwa ambapo saratani ya matiti na shingo ya kizazi zikiongoza.

**38. Mheshimiwa Spika,** Vifo **293 (13%)** kati ya wagonjwa **2,295** waliolazwa kutokana na magonjwa ya moyo ikiwemo athari za shinikizo la juu la damu viliripotiwa. Aidha, vifo **101 (5.7%)** vya wagonjwa **1,775** waliolazwa vilivyosababishwa na athari zilizotokana na ugonjwa wa kisukari viliripotiwa. Kwa upande wa ajali za barabarani, majeruhi **2,102** wameripotiwa, kati ya hao **93** sawa na asilimia **4.4** wamefariki dunia.

39. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, visa **29,729** viliripotiwa katika Vituo vya Afya vilivyosababishwa na vifua sugu hususan ugonjwa wa pumu ambapo wagonjwa **244** walilazwa katika hospitali mbalimbali na wagonjwa **2 (0.8%)** waliripotiwa kupoteza maisha. Kwa upande wa maradhi ya seli mundu (Sickle cell disease) wagonjwa **1,317** waliripotiwa kati ya hao **552** walilazwa katika hospitali mbali mbali na vifo **6 (1.1%)** viliripotiwa.

### Huduma za Ufuatiliaji na Uratibu wa Maradhi ya Miripuko na Dharura za Kiafya

40. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, asilimia **90** ya taarifa za maradhi ya miripuko zimepatikana kikamilifu kama ilivyopangwa. Hata hivyo, ni asilimia **77** tu ya ripoti hizi zilizopatikana kwa wakati. Taarifa hizo zimehusisha miripuko minne **(4)** ikiwemo M-pox, Homa ya Mafua Makali, athari za kula chaza na athari za kula samaki aina ya papa. Wizara inaendelea kuimarisha mifumo yake ili kuhakikisha taarifa zinapatikana kwa usahihi na kwa wakati.

### Huduma za Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kufanya tathmini ya maradhi ya matende na mabusha kwa wanafunzi (Transmission Assessment Survey (TAS), ambapo Wanafunzi **12,608** (Unguja **7,462** na Pemba **5,133**) wenye umri kati ya miaka 6-7 kutoka Wilaya **9** (Unguja **5** na Pemba **4**) walifanyiwa uchunguzi wa maradhi ya matende na

mabusha. Kati yao wanafunzi **11** (Wanaume **8** na Wanawake **3**) sawa na asilimia **0.09** waligundulika kuwa na viashiria vya ugonjwa wa matende na mabusha. Hatua za utoaji wa dawa kinga katika skuli hizo umendelea ili kuweza kuwakinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti na kutokomeza maradhi yasiopewa Kipaumbele, watu **1,031** (Unguja **680** na Pemba **351**) wamechunguzwa maradhi ya kichocho katika vituo vya afya kati ya hao, wagonjwa **714** (Unguja **551** na Pemba **163**) waligundulikana na ugonjwa wa kichocho na kupatiwa matibabu. Aidha wagonjwa **10,811** (Unguja **6,072** na Pemba **4,739**) waligundulika na maradhi ya minyoo ya tumbo (intestinal worms). Kwa upande wa magonjwa ya matende na mabusha, wagonjwa **292** (Unguja **239** na Pemba **53**) waligundulika na kupatiwa matibabu.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kupiga dawa kwenye mito na mabwawa kwa ajili ya kupambana na konokono (Snail Control) wanao eneza maradhi ya Kichocho ili kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo ambapo mabwawa **8** sawa na asilimia **66.7** tayari yameshawekwa dawa kati ya mabwawa **12** yaliyomo kwenye shehia husika.

### Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho

**44.** **Mheshimiwa Spika,** Watu **24,521** (wanaume **1,802** na wanawake **2,075,** na watoto **20,644**) waliochunguzwa na

kupatiwa matibabu ya macho katika Vituo vya Afya vya Unguja na Pemba. Aidha, watu **4,610** (Wanaume **1,759** na Wanawake **2,851**) walichunguzwa na kutibiwa afya zao za macho katika Vijiji **11** Unguja kupitia huduma za mkoba (Outreach Screening). Vile vile, kambi ya uchunguzi wa macho ilifanyika katika hospitali ya Kivunge kwa kushirikiana na Shirika la Specsavers la Norway ambapo watu **1,413** (wanawake **851**, wanaume **551** na watoto **11**) walichunguzwa na kuonekana na uhakiki mbaya wa mwanga machoni (Refractive errors and Presbyopia) na kupatiwa miwani.

45. **Mheshimiwa Spika,** Skuli **10** kutoka Kisiwa cha Pemba zilifanyiwa uchunguzi wa macho ambapo Wanafunzi **2,022** walichunguzwa. Matokeo yalibaini kuwa Wanafunzi **106** (Wanawake **60** na Wanaume **46**) walibainika na matatizo ya uhakiki mbaya wa mwanga machoni na kupimwa miwani. Wanafunzi **11** (Wanawake **6** na Wanaume **5**) walipewa rufaa katika Hospitali za Wilaya kwa matibabu zaidi. Aidha, Wananchi **496** (Wanawake **261** na Wanaume **227**) walifanyiwa upasuaji katika Kambi za upasuaji wa mtoto wa Macho zilizofanyika katika Hospitali ya Vitongoji Pemba na Kituo cha Afya Kizimkazi ambapo wananchi walipata faraja ya kurejeshewa uoni wa macho na sasa wanaendelea na shughuli zao za kimaisha.

### Huduma za Elimu ya Afya

**46. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa elimu ya afya kwenye skuli na taasisi za elimu ya juu ambapo maeneo **174** (**154** skuli za Msingi na Sekondari, **16** Madrasa na **4** Vyuo vikuu) ikijumuisha wanafunzi **76,505** (Unguja **49,536** na Pemba **26,969**) waliopatiwa elimu ya afya. Aidha, vipeperushi **329,522** vyenye ujumbe mbalimbali wa kinga na elimu ya Afya ikiwemo vya maradhi ya M-pox, Ebola, Chanjo na Uharo mkali vilitengenezwa na kusambazwa katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba. Vielimishaji hivyo vilijumuisha vipeperushi na vipindi vya Afya **365** (Radio **267** na TV **98**) viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia vyombo mbalimbali kwa kushirikiana na vitengo vyengine vya Wizara ya Afya.

**47. Mheshimiwa Spika,** Mikutano **249**(Unguja **135** na Pemba **114)** ikijumuisha (**22** Shehia Health Custodian Committee, **33** SACCOS, **66** CHWs, **33** RCCE na **95** madrasa za kina mama) ilifanyika katika shehia mbalimbali Unguja na Pemba ili kuwapatia wanajamii uelewa kuhusu kinga dhidi ya maradhi ya mlipuko. Aidha Shehia **256** zimefikiwa Unguja na Pemba.

**48. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuimarisha **Kituo cha Mawasiliano ya Afya (Call Center)** ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na maradhi ya miripiko na dharura za kiafya ili iweze kuchukuwa hatua stahiki na

kwa wakati. Simu **2,404** (**2,133** jamii, **271** M-mama kati ya hizo **225** rufaa za mama na **46** rufaa za mtoto) zilipokelewa kutoka kwa jamii na kutoa msaada wa dharura kwa mama na mtoto.

### Huduma za Uratibu wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (CHW)

**49. Mheshimiwa Spika;** Wahudumu wa Afya **1,054** (Unguja **753** na Pemba **301**) wamepatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo ya kutoa huduma ya afya ngazi ya jamii. Mafunzo hayo yametolewa kwa muda wa miezi sita. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wahudumu hao ili waweze kutoa huduma za afya ikiwemo za uelimishaji na huduma za afya za awali katika jamii zao. Aidha, wahudumu wa afya **446** (Unguja **300** Pemba **146**) wamelipwa posho zao na wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali Unguja na Pemba. Katika hatua nyengine wahudumu wa afya ngazi ya jamii **1,242** (Unguja **903** na Pemba **339**) waliweza kupatiwa posho zao za mwezi kulingana na utendaji wa kazi zao.

### Huduma ya Afya ya Mazingira

**50. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha ubora na usalama wa maji, Wizara imefanikiwa kutoa vidonge **3,006** (Unguja **1,291** na Pemba **1,715**) vya kutibu maji ambavyo vimegawiwa kwa wananchi wenye uhitaji na visima binafsi. Aidha, vidonge **701,850** (Unguja **564,920** na Pemba

**136,930**) vimegawiwa kwa wananchi wasiopata maji yaliyotibiwa ili waweze kutibu maji majumbani. Jitihada hizi ni endelevu katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi ili kuzuia miripuko ya magonjwa.

**51.** **Mheshimiwa Spika,** Sampuli **63** za maji zimechukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara. Matokeo ya uchunguzi huo yameonesha kuwa sampuli **35** sawa na asilimia **55.5** ya sampuli zilizofanyiwa uchunguzi zimegundulika kuwa hazikuwa salama. Hatua stakihi zilichukuliwa kwa kuwapatia elimu juu ya namna ya kutibu maji kabla ya kuyatumia na kugawa vipeperushi vya elimu kuhusu kutibu maji na ugawaji wa vidonge vya water guard maeneo husika.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na ukaguzi wa kaya, ambapo kaya **60,891** (Wilaya ya Wete **43,475** na Micheweni **17,416**) zilikaguliwa. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kuwa kaya **54,681** (Wete **39,474** na Micheweni **15,207**) sawa na asilimia **90** ndio zenye vyoo. Wizara inaendelea kutoa elimu ya umuhimu wa kujenga na kutumia vyoo bora na salama katika jamii

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kupunguza changamoto ya uhaba wa huduma ya maji katika vituo vya afya na kujenga uhimilivu juu ya athari za mabadiliko ya tabia nchi, Wizara imefanikiwa kufunga miundombinu ya mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua katika vituo vya afya **6** (Unguja **3** na Pemba **3**) vilivyopo maeneo yenye uhaba wa maji. Vituo

vilivyojengwa na kufungiwa miundombinu hiyo ni Kinyikani, Maziwani, Tumbe Maafa, Chaani Masingini, Tumbatu Gomani na Bumbwini Makoba. Ili kuitunza na kuilinda miundombinu hio wafanyakazi wa vituo husika, uongozi wa Shehia na jamii iliyozunguka maeneo ya vituo walipatiwa mafunzo.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za afya katika vituo vya afya na hospitali, tani **477.4** (Unguja tani **397.6** na Pemba tani **77.8**) zimekusanywa na kuangamizwa katika matanuri ya taka yaliyopo Kibele Unguja na Vitongoji Pemba.

**Huduma za Afya ya Mipakani (Bandarini na Viwanja vya ndege)**

55. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za afya mipakani, vyombo vya usafiri **45,245** vilivyoingia nchini vilikaguliwa, kati ya hivyo **36,188** vya anga na **9,057** vya baharini. Vyombo **15** vya baharini vilibainika kuwa havijakidhi vigezo vya afya vya kimataifa ambavyo vilichukuliwa hatua zikiwemo kupatiwa elimu ya afya juu ya usafi wa mazingira na kuruhusiwa kuondoka.

56. **Mheshimiwa Spika,** Wasafiri waliongia nchini na kukaguliwa ni **5,564,081** kati ya hao **4,803,515** walikua wenyeji na **760,566** walikuwa ni wageni, ambapo wasafiri **34** (**15** Wageni na **19** Wenyeji) walibainika kuwa na joto

kubwa la mwili zaidi ya nyuzi joto **38** walipofanyiwa uchunguzi wa awali, baada ya kufanyiwa upimaji joto wa marejeo watu **5** ambao ni wenyeji waligundulika na malaria na walipatiwa huduma ya kwanza na kuripotiwa kama miongozo inavyoelekeza, na waliobaki walibainika kuwa na joto la kawaida kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ya joto na uchovu wa safari.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutoa chanjo kwa wasafiri wa nje ya nchi, wasafiri **5,497** (Unguja **5,025** na Pemba **472**), kati ya hao, wasafiri (wanaume ni **2,634** na wanawake ni **2,863**) wamepatiwa chanjo. Aidha, wagonjwa **903** na maiti **296** walipitishwa na kukaguliwa Bandarini na Viwanja vya Ndege. Katika ukaguzi huo hakukua na maiti wala wagonjwa waliogundulika na magonjwa ya kuambukiza.

**Huduma za Afya ya Wafanyakazi**

**58.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, wafanyakazi **38,282 (**Unguja **33,703** na Pemba **4,579)** walichunguzwa afya zao ukilinganishwa na wafanyakazi **38,158 (**Unguja **35,091** na Pemba **3,067)** waliochunguzwa kwa mwaka 2024/2025 wakijumuishwa wafanyakazi wa Serikali, wafanyakazi katika sekta binafsi, wanafunzi, wafanyabiashara za vyakula, mabaharia pamoja na wafanyakazi wanaosafiri nje ya nchi. Wafanyakazi **1,855** (Unguja **1,429** na Pemba **426**) waligundulika na matatizo

ya kiafya ikijumuisha Homa ya Ini **B** na **C**, maradhi ya kujamiana pamoja na maambukizi ya mfumo wa njia ya mkojo.

### Huduma za Afya ya Msingi ya Akili

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeimarisha huduma za afya ya msingi ya akili kwa kuendelea kujengea uwezo watoa huduma **33** (Madaktari **10**, Afisa tabibu **16** na Wauguzi **7**) kwa ajili ya kutibu magonjwa ya akili. Watu **18,476** (Wanaume **6,763** na Wanawake **11,713**) wamechunguzwa kati yao **457** waligundulika kuwa na viashiria vya magonjwa ya akili na **33** walipata rufaa kwa huduma za kitaalamu zaidi.

### Huduma za Damu Salama

**60.** **Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya mifuko ya damu **14,979** sawa na asilimia **99.8** ya lengo ambapo ilipangiwa kukusanya mifuko ya damu **15,000**. Kati ya hizo, mifuko **8,819** sawa na asilimia **58.9** walikuwa wachangiaji wapya na mifuko **6,160** sawa na asilimia **41.1** zilipatikana kutoka kwa wachangiaji wanaorudia.

### Huduma za Maabara ya Afya ya Jamii

**61.** **Mheshimiwa Spika,** Huduma za maabara ya afya ya jamii zinaendelea kuwa mhimili muhimu katika kuimarisha

utambuzi wa magonjwa, ufuatiliaji wa miripuko, na kufanya maamuzi sahihi ya kiafya hapa Zanzibar. Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuwekeza katika kuimarisha huduma hizi ili kuhakikisha zinakuwa bora, sahihi na zinazoaminika.

62. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, sampuli **1,469** zilipokelewa kutoka vituo vya afya Unguja na Pemba kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa ya miripuko, ikiwemo sampuli **1,308** za washukiwa wa Mafua Makali na UVIKO-19, sampuli **131** za washukiwa wa Ugonjwa wa M-pox, na sampuli **30** za washukiwa wa Homa ya Dengue. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa sampuli za washukiwa **258** ziligundulika na maambukizi ya Mafua Makali kati ya **1,308**, sampuli za washukiwa **47** kati ya sampuli **131** ziligundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa M-pox. Kwa upande wa Homa ya Dengue matokeo yalionesha kuwa hapakuwa na sampuli zilizogundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa Homa ya Dengue. Wagonjwa wote waliogunduliwa wametibiwa katika vituo vya afya na kupona.

## G. PROGRAMU KUU: HUDUMA ZA TIBA (PH0102)

63. **Mheshimiwa Spika,** Progamu hii ina jukumu la kuhakikisha jamii inapata huduma bora za tiba katika Hospitali za Wilaya na Mikoa. Utekelezaji wa shughuli za Programu hii imegawika katika program ndogo mbili ambazo ni Huduma za Matibabu na Huduma za Uchunguzi.

**64. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **TZS 207.06 bilioni** kati ya hizo **TZS 22.77 bilioni** kwa ajili ya mishahara, **TZS 62.84 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 9.74 bilioni** kwa ajili ya Ruzuku na **TZS 111.71 bilioni** (**TZS 48.32 bilioni** kutoka Serikalini, **TZS 63.39 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS 37.53 bilioni** ni Msaada na **TZS 25.86 bilioni** mkopo) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**65. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 100.74 bilioni** sawa na asilimia **65** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 15.71 bilioni** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 59.93 bilioni** matumizi mengineyo na **TZS 5.02 bilioni** ni Ruzuku. Kwa upande wa fedha za maendeleo, **TZS 20.08 bilioni** sawa na asilimia **18** zilipatikana. Kati ya fedha hizo **TZS 16.46 bilioni** sawa na asilimia **38** kutoka Serikalini na **TZS 3.62 bilioni** sawa na asilimia **5** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS 3.46 bilioni** ni Msaada na **TZS 0.16 bilioni** mkopo). Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu katika hospitali za wilaya na mkoa;

ii. Kuimarisha kambi za matibabu na mashirikiano ya huduma za afya kimataifa;

iii. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa tiba na vitendanishi;

iv. Kuimarisha huduma za uchunguzi (maabara na radiolojia);
v. Kuimarisha usimamizi katika uhifadhi na utumiaji wa dawa na vifaa vya utibabu katika hospitali na vituo vya afya;
vi. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wahanga wa udhalilishaji;
vii. Kuimarisha uratibu wa huduma za uuguzi na ukunga;
viii. Kuimarisha huduma za tiba kwa mashirikiano na sekta binafsi;
ix. Kuimarisha udhibiti wa chakula, dawa na vipodozi; na
x. Kuimarisha uchunguzi na udhibiti wa sumu, kemikali na vinasaba.

## H. PROGRAM NDOGO: HUDUMA ZA MATIBABU (SH010201)

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina jukumu la kusimamia utoaji wa huduma za tiba na uangalizi wa wagonjwa katika Hospitali za Wilaya, Mkoa na Rufaa huduma za afya pamoja na ufuatiliaji wa ubora wa huduma za matibabu, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na huduma za uchunguzi ili kuimarisha afya na ustawi wa jamii.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 huduma hii ilipangiwa **TZS 194.49 bilioni** kati ya hizo **TZS 22.77 bilioni** kwa ajili ya Mishahara, **TZS 62.84 bilioni** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **TZS 2.97 bilioni** Ruzuku kwa Taasisi **(TZS 1.77 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS 1.20 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo) na **TZS 105.91 bilioni** (**TZS 42.52 bilioni** kutoka Serikalini, **TZS**

**63.39 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS 37.53 bilioni** ni Msaada na **TZS 25.86 bilioni** mkopo) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

68. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 96.87 bilioni** sawa na asilimia **66** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 15.71 bilioni** Mishahara, **TZS. 59.93 bilioni** Matumizi Mengineyo na **TZS 1.15 bilioni** Ruzuku kwa Taasisi **(TZS 0.98 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS 0.16 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo). Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo **TZS 20.09 bilioni** zilipatikana (**TZS 16.46 bilioni** Kutoka Serikalini, **TZS 3.63 bilioni** Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS 3.46 bilioni** Msaada na **TZS 0.16 bilioni** Mkopo).

**Huduma za Uchunguzi wa Maradhi**

69. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za uchunguzi ni huduma zinazojumuisha uchunguzi wa maradhi kwa kutumia sampuli za aina mbalimbali zinazotokana na binaadamu. Uchunguzi hufanyika kwa njia picha (Radiology and Imaging Services) zikiwemo X-ray, Ultrasound, CT scan na MRI. Huduma hizi hutolewa katika hospitali za Serikali na zile za binafsi. Mpaka kufikia Machi 2026, Wizara imefanikiwa kupima vipimo **1,661,661** kwa wagojwa. Kati ya hivyo maabara ni **1,474,444** (Unguja **1,035,074** na Pemba **439,370**), kwa njia ya picha **187,217** (Unguja **127,904** na Pemba **59,313**). **Kiambatisho 4a kinafanua zaidi**

**Huduma za Matibabu**

**70. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imefanya kambi za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ambapo huduma za matibabu ya wagonjwa wa nje na wagonjwa waliolazwa ziliendelea kutolewa katika Hospitali za Wilaya, Mkoa na Hospitali za Rufaa za Taifa na Binafsi. Mahudhurio ya wagonjwa wa nje ni **925,748** (wanaume **369,322** na wanawake **556,426**) na wagonjwa waliolazwa ni **79,475** (wanaume **27,764** na wanawake **51,711**). Aidha, wagonjwa **1,899** (wanaume **1,052** na wanawake **847**) wamefariki dunia. Sababu kuu ya vifo hivyo ni pamoja na maradhi ya moyo, kiharusi, saratani, kisukari, vifo vya watoto wachanga na vifo vinayvotokana na ajali za barabarani. Wagonjwa **180** wanaendelea kupata huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa Figo "Dialysis" ambapo wagonjwa **35** wamepatiwa huduma katika Hospitali ya Abdulla Mzee na wagonjwa **145** walipatiwa huduma hio katika Hospitali ya Rufaa ya Lumumba. **Kiambatisho 4b kinafanua**

**Huduma za Ushirikiano wa Afya Kimataifa**

**71. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imefanya kambi za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ambapo kambi **15** (**10** Unguja na **5** Pemba) zimefanyika katika hospitali za Wilaya na Mkoa. Aidha, Wagonjwa **763** walipatiwa huduma za upasuaji kati ya hao, **302** upasuaji

wa jumla kwa watoto na watu wazima, **312** magonjwa ya kina mama, **149** magonjwa ya mfumo wa mkojo. Aidha idadi ya kambi inaonekana kupungua kwa mwaka 2025/ 2026 ikilinganishwa na kambi **22** za uchunguzi na matibabu zilizofanyika kwa mwaka 2024/2025 ambapo wagojwa **12,050** walipatiwa matibabu ya maradhi mbalimbali kufuatia uchunguzi katika kambi hizo.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Wagonjwa **570** walisafirishwa nje ya Zanzibar ambapo wagonjwa **101** walisafirishwa na kutibiwa nje ya Tanzania (India **65**, na Israel **36**). Aidha wagonjwa **138** walipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, **95** Taasisi ya Mifupa MOI, **108** Jakaya Kikwete Cardiac Institute, **72** Kilimanjaro Christian Medical Centre na **92** Ocean Road Cancer Institute. Takwimu hizi zimeonyesha kuongezeka kwa wagonjwa wanaopewa rufaa nje ya Zanzibar kutoka rufaa **407** mwaka 2024/2025. Ongezeko hili limechangiwa zaidi na kuwa wagonjwa wengi wanafika hospitali wakiwa katika hatua za mwisho za maradhi na hivyo kuhitaji matibabu ya kisasa zaidi ambayo hayapatikani Zanzibar. **Kiambatisho 4c kinafanua zaidi**

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na changamoto ya ongezeko la wagonjwa wanaopewa rufaa nje ya Zanzibar, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za kinga, huduma za Kibingwa na kibingwa bobezi za matibabu ya mifupa (upandikizaji wa nyonga na magoti bandia), Moyo (uchunguzi na matibabu ya mishipa ya moyo ilioziba "Cath

lab") katika hospitali ya Mkoa ya Lumumba. Hatua nyengine ni kuimarisha miundombinu ya Afya ikiwemo ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia Binguni, Hospitali ya Saratani Binguni, Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na kuanzisha vituo mahiri vya mafunzo ya madaktari bingwa na bobezi kupitia vyuo vya Jumuiya ya Afya ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini (ECSA) ambapo kituo kimoja **1** kimeanzishwa Hospitali ya Rufaa ya Wilaya Mwera Pongwe (Obstetrics and Gynaecology) na **2** vimekamilisha maombi ya awali ambavyo ni Hospitali ya Lumumba (General Surgery and Anaesthesia) na Hospitali ya Ijtimai (Obstetrics and Gynaecology.)

**Huduma ya Mkono Kwa Mkono (One Stop Centre)**

**74. Mheshimiwa Spika,** Wahanga **1,389** (Wanaume **230** na Wanawake **1,159**) wa matukio ya ukatili wa kijinsia yaliripotiwa katika vituo vya afya na hospitali ambapo matukio hayo yamejumuisha udhalilishaji wa kimwili **68**, udhalilishaji wa kihisia **65**, ubakaji **469**, ulawiti **199**, ubakaji na ulawiti **230**, kukashifiwa **74**, mimba za utotoni **146** na jaribio la kubakwa na kulawitiwa **138**. Wizara inaendelea na jitihada za utoaji wa elimu na ushauri nasaha kwa wahanga wa matukio hayo. Takwimu hizi zinaonesha kwamba visa hivi vimepungua ikilinganisha na mwaka 2024/2025. **Kiambatisho 4d kinafanua zaidi.**

## Huduma za Bodi na Mabaraza ya Taaluma za Afya

### Baraza la Madaktari

**75. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia usajili, utendaji na maadili ya wataalamu pamoja na taaaluma ya udaktari kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Hadi kufikia Machi, Baraza la Madaktari limefanikiwa kusajili Madaktari **2,430** kati ya hao, Madaktari wapya walosajiliwa ni **562** na **1,868** wamehuisha leseni zao. Katika kuhakikisha maadili ya kulinda taaluma na kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa hatua za kinidhamu zimekuwa zikichukuliwa kwa madaktari wanaokiuka maadili ya taaluma zao ambapo madaktari **20** walipatiwa adhabu mbalimbali ikiwemo kuzuia leseni **2**, kupewa onyo la maandishi **7**, kufutiwa leseni **10** na daktari mmoja aliwasilishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi baada ya kubainika kuwa alikuwa akifanya kazi Zanzibar bila ya kuwa na usajili halali wa Baraza, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Sheria.

### Baraza la Wataalamu wa Maabara za Tiba

**76. Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia usajili, utendaji na maadili ya wataalamu wa maabara kwa mujibu wa sheria, Kanuni na taratibu, wataalamu wa Maabara za tiba **716** walisajiliwa na kuhuwishwa leseni zao, kati ya hao wataalamu wapya **286** (**62** Shahada ya Kwanza na **224** Diploma) walisajiliwa na kupatiwa leseni na wataalamu **430** walihuwisha leseni zao (**252** Unguja na **178** Pemba).

**Baraza la Wauguzi na Ukunga**

**77. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wauguzi na Wakunga limefaninikiwa kusajili na kutoa leseni kwa Wauguzi na Wakunga **978,** kati ya hao wauguzi na wakunga wapya waliosajiliwa ni **419**. Vile vile, Wauguzi na wakunga **559** wamehuisha leseni zao. Katika kuhakikisha maadili ya kulinda taaluma na kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa hatua za kinidhamu zimekuwa zikichukuliwa kwa wauguzi na wakunga ambao wamekiuka maadili ya taaluma yao ambapo wauguzi na wakunga **2** wamesimamishiwa leseni zao kwa muda wa miezi sita na **3** wamefikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi baada ya kubainika kuwa walikuwa akifanya kazi Zanzibar bila ya kuwa na usajili halali wa Baraza, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Sheria.

**Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi**

**78. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2026, Wizara imepokea maombi ya usajili wa Vituo vya Afya **29** vya afya binafsi kati ya hayo; maombi **12** yamepewa usajili, maombi **4** yamekataliwa kutokana na kuwepo katika maeneo yasiyofaa na maombi **13** yanaendelea na marekebisho. Katika hatua nyengine, Wizara imefanya ukaguzi wa vituo vya Afya na hospitali binafsi **163** (Unguja **148**, Pemba **15**). Matokeo ya ukaguzi huo kituo kimoja (**1**) kilifungiwa kutokana na kutokidhi vigezo, kukosa wafanyakazi na kutokufanya marekebisho kwa wakati uliotakiwa na vituo

**13** vilipewa adhabu kutokana na kuendesha hospitali bila ya kuwa na leseni halali, kutoa huduma nje ya wigo, kuajiri wafanyakazi ambao hawana sifa (hawajasajiliwa) na kutoa huduma chini ya viwango kwa kutofuata njia za kuzuia maambukizi (IPC).

**Baraza la Taaluma za Afya ya Jamii na Mazingira**

**79. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha wataalamu wa Afya ya Mazingira wanazingatia maadili, sheria na miongozo ya taaluma zao. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Baraza limeweza kusimamia taaluma za kada ya Afya ya Jamii na Mazingira kwa kutoa usajili na leseni za kazi kwa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira. Baraza limesajili Maafisa Afya wa Mazingira **37** sawa na asilimia **93** ya lengo la kusajili maafisa wa Afya wapya **40** Aidha, Maafisa **344** sawa na asilimia **86** ya lengo la **400** walihuisha leseni zao. Baraza limeendesha mafunzo ya utarajali (internship) kwa wahitimu **66** (**61** Unguja na **5** Pemba) wa kada za afya ya jamii na mazingira.

**Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala**

**80. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala limefaninikiwa kusajili na kutoa leseni kwa kliniki za tiba asili **63**, kliniki za tiba mbadala **11**, maduka ya dawa asili **295**, waganga wa tiba asili **616** na wasaidizi waganga Wauguzi **260** na ghala za kuhifadhia dawa **2**. Sambamba na hilo, Wizara imefanya ukaguzi kwa vituo vya tiba asili na

tiba mbadala **224** (Unguja **177** na Pemba **47**). Matokeo ya ukaguzi huo maduka **5** Unguja yamefungiwa kutokana na makosa ya ukiukwaji wa taratibu za kisheria ikijumusha kutokuwa na usajili wa baraza na kutohuisha leseni.

**81.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imepiga hatua katika usafirishaji na uingizaji wa dawa asili ambapo hati **8** za kusafirisha dawa nje ya Zanzibar zimetolewa baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kiusalama. Dawa hizo zilisafirishwa kwenda Uingereza, Marekani na Kanada. Vilevile, leseni **1** ya uingizaji wa dawa asili kutoka India imetolewa.

**Huduma za Uuguzi na Ukunga**

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya ukaguzi katika Vituo vya Afya **150** (**95** Unguja **55** Pemba) ambapo matokeo ya ukaguzi huo yalionyesha kuimarika kwa utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga, kuongezeka kwa uzingatiaji wa viwango vya ubora wa huduma, pamoja na ufuatiliaji mzuri wa mifumo ya utoaji wa huduma katika vituo vya afya.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, ukaguzi ulifanyika katika hospitali za Wilaya **12** (**8** Unguja na **4** Pemba), matokeo ya ukaguzi yalionyesha kuwa mwenendo mzuri wa ongezeko la viwango vya utendaji kutoka wastani wa asilimia **63.6** kwa mwaka 2024 hadi kufikia wastani wa asilimia **84.2** kwa mwaka 2025. Aidha, matokeo hayo yameonesha kuongezeka kwa uzingatiaji wa kufuata miongozo ya kutoa huduma, pamoja na mafanikio ya hatua za usimamizi na ufuatiliaji zinazoendelea kufanywa na Wizara.

**Huduma ya Upatikanaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi;**

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali imekadiriwa **TZS 18.10 bilioni** kutoka Serikalini kwa ajili ya ununuzi wa dawa muhimu na vifaa tiba kwa afya ya msingi na programu. Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 7.42 bilioni** zimetumika sawa na asilimia **55** ya makadirio ya **TZS 13.57 bilioni.**

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuboresha Hali ya upatikanaji wa dawa na Vifaa Tiba hadi kufikia Machi 2025 kwenye Hospitali za Mikoa na Wilaya. Hali ya upatikanaji imevuka malengo ya asilimia **95** na kufikia asilimia **97**, na kwenye vituo vya Afya ngazi ya Msingi imeshuka kutoka asilimia **84** hadi kufikia asilimia **81**. Hali hii imetokana na mabadiliko ya mfumo wa ugharamiaji wa dawa na vifaa tiba uliokuwepo awali. Hata hivyo hali hii imeshaimarika kwa sasa imefikia asilimia **92**. Serikali itaendelea kutoa kipaombele katika upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba katika vituo vya Afya na Hospitali.

**Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa**

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina jukumu la kuhakikisha uzalishaji uhifadhi na usambazaji, kwa kuimarisha upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba vyenye ubora kwa wakati. Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, huduma hii ilipangiwa

**TZS 2.97 bilioni** kati ya hizo **TZS 1.77 bilioni** kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara, **TZS 1.20 bilioni** kwa ajili ya Ruzuku ya Matumizi Mengineyo.

**87. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 1.15 bilioni** sawa na asilimia **52** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 0.99 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS 0.16 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo.

**88. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa ilinunua Dawa, Vitendanishi vya Maabara na vifaa tiba kutoka kwa wazalishaji na wazabuni yenye thamani ya **TZS 9.07 bilioni** na kusambazwa katika vituo vya Afya Unguja na Pemba.

**89. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa imeuza Dawa na Vifaa tiba kwa kila mwezi katika maeneo **221** (Unguja **136** na Pemba **85**) ya usambazaji (Distribution Points) ya Umma, ambapo bidhaa zilizosambazwa kwenye vituo vya Umma katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, zilikua na thamani ya shilingi **7.42 bilioni**

**90. Mheshimiwa Spika,** Wizara imezalisha hewa tiba (Oxygen) kupitia Mitambo mitatu **(3)** ya Hewa tiba ya Lumumba, Mwera Pongwe na Vitongoji. Aidha, lita **1,525,790** (lita **1,442,732** hospitali za umma na lita **83,058** hospitali binafsi) zilizalishwa na kusambazwa.

## I. PROGRAM NDOGO: HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH010202)

**91. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (Chief Government Chemist Laboratory Agency). Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **TZS. TZS 12.57 bilioni** kati ya hizo **TZS 6.77 bilioni** Ruzuku kwa Taasisi (**TZS 5.46 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS 1.31 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo) na **TZS 5.80 bilioni** kutoka Serikalini kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**92. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 3.87 bilioni** sawa na asilimia **41** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 3.66 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS 0.21 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo.

**Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi**

**93. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ina jukumu la kusimamia na kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa Chakula, Dawa, Vipodozi, Vifaa tiba na Vitendanishi kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi nambari **2/2006** na marekebisho yake ya Sheria nambari **3/2017**.

**94. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wakala ilipangiwa **TZS 5.57 bilioni** kati ya hizo **TZS 3.37**

**bilioni** kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara na **TZS 2.20 bilioni** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 2.21 bilioni** sawa na asilimia **53** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana ambazo ni Malipo ya Mishahara.

**95. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Wakala imefanikiwa kuchunguza sampuli **944** zikiwemo Chakula **708**, Dawa **141**, Vipodozi **73** na Vifaa Tiba **22.** Matokeo ya uchunguzi yameonesha kuwa sampuli **217** (Chakula **215**, Kipodozi **1** na Kifaa Tiba **1**) hazikufikia viwango vilivyowekwa na havifai kwa matumizi ya binaadamu.

**96. Mheshimiwa Spika,** Wakala imefanya ukaguzi wa majengo ya biashara za bidhaa za Chakula, Dawa, Vipodozi na Vifaa tiba **3,162** (Unguja **2,493** na Pemba **669**). Matokeo ya ukaguzi huo yameonesha kuwa maduka **82** yalifungwa kutokana na kukiuka utaratibu uliowekwa Unguja yakiwemo ya dawa **71** na vipodozi **10** na chakula **1**. Aidha, kufuatia ukaguzi na uchunguzi wa bidhaa wakala imeteketeza tani **229.33** za bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu zikiwemo za chakula tani **222.83**, dawa **4.5** na vifaa tiba **2**

**97. Mheshimiwa Spika,** Majengo **846** (Unguja **765** na Pemba **81**) ya biashara za bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba yamesajiliwa. Vile vile, maombi ya usajili wa bidhaa **117** yalipokelewa kati ya maombi hayo maombi **34** (chakula **19**, dawa **1**, kipodozi **1** na vifaa tiba **13**) yamesajiliwa baada ya kuonekana yamekidhi vigezo vya usajili. Aidha, maombi

**3** yote ya chakula yamekataliwa na maombi **66** (Chakula **43**, Vipodozi **23**) yanaendelea na uchambuzi na kukamilisha taratibu za usajili. Katika hatua nyengine Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi imefanikiwa kuwa mwanachama wa mtandao wa Mamlaka za Udhibiti wa Dawa barani Afrika (African Medicines Agency-AMA) chini ya Umoja wa Afrika (African Union).

**Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (Chief Government Chemist Laboratory Agency) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Maabara nambari **10/2011**. Lengo kuu la maabara hii ni kutoa huduma za uchunguzi wa kisayansi ya jinai, sampuli za kemikali na mazingira, pamoja na sampuli za chakula na dawa.

**99.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wakala ilipangiwa **TZS 7.00 bilioni** kati ya hizo **TZS 2.09 bilioni** kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara, **TZS 1.31 bilioni** kwa ajili ya Ruzuku ya Matumizi Mengineyo na **TZS 3.60 bilioni** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**100.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 1.65 bilioni** sawa na asilimia **32** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 1.45 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS 0.20 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo.

101. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, sampuli **2,175** zilifanyiwa uchunguzi katika Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar. Kati ya sampuli hizo, sampuli **1,730** zilikuwa za uchunguzi wa makosa ya jinai, sampuli **150** zilikuwa za kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali na sampuli **295** zilikuwa za chakula na dawa.

102. **Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchunguzi huo yanaonesha kuwa sampuli **2,044** zilikidhi viwango vinavyotakiwa, Sampuli **131** hazikukidhi viwango vilivyowekwa. Kutokana na hali hiyo, hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwemo kutoa elimu na ushauri kwa wateja na wadau husika ili kuhakikisha biashara na shughuli zao zinaendeshwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

103. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha udhibiti wa kemikali Zanzibar, Wakala ilipanga kutoa vibali **4,386** zinavyohusiana na kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali. Hadi kufikia Machi 2026, vibali **3,398** vimetolewa. Kati ya vibali hivyo, vibali **3,200** ni vya uingizaji wa kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali, vibali **196** ni vya utoaji wa kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali na vibali **2** ni vya usafirishaji wa kemikali. Hatua hii imechangia kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya kemikali ili kuhakikisha usalama wa afya ya jamii na mazingira pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

**104. Mheshimiwa Spika,** Wakala imefanya ukaguzi wa maeneo **311** yanayohifadhi kemikali. Sambamba na hilo, wakala ilisajili maeneo **184** (Unguja **172** na Pemba **12**) ya kuhifadhi kemikali na maeneo **176** yalihuisha hati za usajili.

**105. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha usimamizi na udhibiti wa kemikali Zanzibar, Wakala imefanya ukaguzi wa maeneo **311** (Unguja **294** na Pemba **17**) yanayohifadhi kemikali. Sambamba na hatua hiyo, Wakala ilisajili maeneo **184** ya kuhifadhi kemikali (Unguja **172** na Pemba **12**). Aidha, maeneo **176** yalihuisha hati za usajili, (Unguja **170** na Pemba **6**).

## J. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PH0103)

**106. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya inajumuisha programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afya Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **TZS 57.10 bilioni** kati ya hizo **TZS 35.25 bilioni** kwa ajili ya mishahara na **TZS 11.25 bilioni** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **TZS 2.47 bilioni** kwa ajili ya Ruzuku na **TZS 8.13 bilioni** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka Serikalini.

**107. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 32.53 bilioni** sawa na asilimia **76** ya makadirio ya miezi tisa

zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 24.33 bilioni** Mishahara na **TZS 4.87 bilioni** Matumizi Mengineyo na **TZS 1.49 bilioni** Ruzuku kwa Taasisi (**TZS 1.32 bilioni** Mishahara na **TZS 0.17 bilioni** Matumizi mengineyo). Kwa upande wa Fedha za Maendeleo, **TZS 1.84 bilioni** zilipatikana Kutoka Serikalini kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa na kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

ii. Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa Sera, Sheria na Miongozo ya utoaji huduma za afya;

iii. Kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano wa kugharamia huduma za afya;

iv. Kufanya tafiti, ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya;

v. Kuimarisha mifumo ya kidigitali ya taarifa za afya;

vi. Kuimarisha miundombinu ya huduma za afya ikiwemo matengenezo ya majengo na vyombo vya usafiri;

vii. Kuratibu utekelezaji wa mfumo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma;

viii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya afya Pemba; na

ix. Kuratibu na kufanya tafiti mbalimbali za afya.

## K. PROGRAMU NDOGO: UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301)

**108. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kuweka mazingira bora ya kiutawala na kiutendaji ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Wizara. Programu hii husimamia masuala ya utawala wa rasilimali watu, fedha, manunuzi, mawasiliano, Sheria, TEHAMA, Ukaguzi wa ndani na huduma za ofisi na usafiri. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **TZS 19.70 bilioni** kati ya hizo **TZS 7.13 bilioni** kwa ajili ya Mishahara na **TZS 5.97 bilioni** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **TZS 6.60 bilioni** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka Serikalini.

**109. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 10.86 bilioni** sawa na asilimia **73** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 4.82 bilioni** Mishahara na **TZS 4.20 bilioni** Matumizi Mengineyo na **TZS 1.84 bilioni** Miradi ya Maendeleo kutoka Serikalini

### KUIMARISHA NGUVU KAZI KWA SEKTA YA AFYA

**110. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Wizara ya Afya ina wafanyakazi **8,448** (Unguja **6,122** na Pemba **2,326**). Wizara imeajiri wafanyakazi **67** wa kada mbalimbali. Wafanyakazi **116** wa kada mbalimbali wamerudi kutoka masomoni. Sambamba na hilo Wizara imepeleka masomoni wafanyakazi **237**. Aidha, wafanyakazi **67** wamejiunga na

mafunzo ya Utarajali (Intenship) katika Hospitali na Vituo vya Afya mbalimbali. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi (Saifee Hospital na NSK) imeweza kuajiri wafanyakazi **(605)** katika kada mbalimbali, ikiwemo madaktari **143(Daktari Bingwa 28)** wauguzi **208(Wauguzi Bingwa 25)**, Wataalam wa usingizi **40, na** Madaktari wa wagonjwa mahututi **4 (Kiambatisho 5a, 5b, 5c na 5d kinafafanua zaidi).**

**111. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa maslahi na stahiki zao wafanyakazi **410** wamelipwa fedha za likizo, wafanyakazi **54** wapewa fedha za Ubani. Aidha, Wafanyakazi **2** wamesimamishwa kazi na **10** wamefukuzwa kazi kutokana na sababu za kinidhamu, wafanyakazi **9** wamestaafu na wafanyakazi **2** wamefariki dunia Mungu azilaze roho zao peponi. Amin.

## URATIBU WA MANUNUZI, FEDHA NA UKAGUZI WA WIZARA

**112. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, mikataba **3** ya zabuni ya Washauri Elekezi imekamilika na baadhi ya washauri elekezi wameanza kazi kwa ajili ya kusimamia miradi mbalimbali ya ujenzi ikiwemo: -

i. Ujenzi wa Maabara ya Afya ya Jamii Zanzibar eneo la Dunga;

ii. Ujenzi wa Hospitali ya Saratani eneo la Binguni;

iii. Ujenzi wa Hospitali za Mikoa, Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba, Kusini Pemba na Kusini Unguja; na
iv. Ujenzi wa Vituo vya Afya sita (**6**) Mombasa, Mwera Mtofaani, Bumbwini Misufini, Magirisi kwa upande wa Unguja, Mkoani RCH na Madungu kwa upande wa Pemba.

**113. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za rufaa kwa wagonjwa pamoja na shughuli za ufuatiliaji wa huduma za afya katika jamii, Wizara imefanya ununuzi wa gari ishirini na tisa (**29**), basi moja (**1**) na pikipiki nne (**4**). Hatua hii itaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za afya, kurahisisha usafirishaji wa wagonjwa wa rufaa, pamoja na kuimarisha shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa huduma za afya katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

**HUDUMA ZA AFYA KIDIJITALI**

**114. Mheshimiwa Spika,** Katika kurahisisha ubora wa mawasiliano ya kimtandao na kuwezesha matumizi ya mifumo ya kidijitali kwenye Vituo vya Afya, Wizara imefanikiwa kuunganisha mkonga kwenye vituo vya afya vya msingi **65** (Unguja **48** na Pemba **17**) kati ya hivyo vituo **19** tayari vimeshaanza kutumia huduma hiyo. Aidha, Katika kukabiliana na changamoto ya kuwa na mifumo mingi ya kidigitali Wizara imepunguza idadi ya mifumo kutoka mifumo **43** hadi kufikia mifumo **23** ambapo lengo ni kuwa na mfumo mmoja tu wa taarifa za Afya Zanzibar (Unified Health Information system).

**115. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha matumizi ya mifumo ya digitali, Wizara imefanya manuuzi ya vifaa **1,015** vya aina mbalimbali na kugawiwa kwenye Vituo vya Afya vya msingi Unguja na Pemba. Vifaa hivyo vinajumuisha Komputa **514** (Unguja **322** na Pemba **192**), Vishkwambi **283** (Unguja **177** na Pemba **106**), Printers **108** (Unguja **72** na Pemba **36**), na UPS **110** (Unguja **74** na Pemba **36**). Sambamba na hilo, Wizara imetoa mafunzo ya mfumo wa Taarifa za Wagonjwa (ZanEMR) kwa watoa huduma **537** wa Vituo vya Afya ngazi ya msingi ili kuwajengea uwezo wa kutumia mfumo huo. Kufuatia mafunzo hayo hadi sasa vituo **77** vya afya ya msingi vinatumia mfumo wa ZanEMR, ambapo vituo **21** kati ya hivyo vinatumia mfumo kwenye maeneo yote ya kutolea huduma.

## L. PROGRAMU NDOGO: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302)

**116. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ikiwemo Mipango ya Kisekta, Ufuatiliaji na Tathmini, Sera, mikakati, Miongozo na Uratibu wa Tafiti za Afya. Aidha, Programu hii inasimamia ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya takwimu na taarifa mbalimbali za Afya kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi ili kuhakikisha utoaji wa huduma unazingatia mahitaji ya wananchi.

117. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **TZS 5.56 bilioni** kati ya hizo **TZS 0.70 bilioni kwa** ajili ya Mishahara, **TZS 0.86 bilioni** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **TZS 2.47 bilioni** Ruzuku kwa Taasisi (**TZS 1.78 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS. 0.69 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo) na **TZS 1.53 bilioni** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka Serikalini.

118. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 2.16 bilioni** sawa na asilimia **52** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TZS 0.60 bilioni** Mishahara na **TZS 0.07 bilioni** Matumizi Mengineyo na **TZS 1.49 bilioni** Ruzuku kwa Taasisi (**TZS 1.32 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS 0.17 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo).

119. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuandaa Mkutano wa Kumi na Tano (**15**) wa mwaka wa Mapitio ya Sekta ya Afya ambao umeshirikisha wadau mbalimbali ili kujadili mafanikio na changamoto za sekta kwa kipindi cha mwaka 2024/2025.

120. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ubora wa huduma za afya katika ngazi zote, Wizara imeanzisha Mfumo wa kieletroniki wa utaoji wa Maoni (ZanAfya Maoni) kwa wananchi wanaofika katika Hospitali na Vituo vya Afya kupata huduma. Mafunzo ya kuutambulisha Mfumo huo

yamefanyika kwa Wakuu wa Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya katika Jamii **143** (**80** Unguja na **63** Pemba) na Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (CHWs) **1,044** (Unguja **735** na Pemba **309**). Hadi kufikia machi 2026, vituo vya afya **166** (Unguja **95** na Pemba **71**) vimeshaanza kupokea maoni ambapo vituo **79** (Unguja **53** na Pemba **26**) vimeshaunganishwa na ZanEMR na tayari kuna dashboard zimeandaliwa ambazo zinazotoa taarifa za matokeo ya mirejesho (feedback) inayotolewa na wananchi. Mfumo huu utasaidia kuimarisha huduma za afya kufuatia mapungufu yanayoripotiwa.

**121. Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia ubora wa viwango na utekelezaji wa mipango kazi ya kufuatilia huduma za afya zinazotolewa katika vituo vya afya na hospitali, Wizara imeanzisha timu za kusimamia ubora na viwango (Quality improvement team). Hadi kufikia Machi 2026, vituo vya afya ya msingi **135** (Unguja **82** na Pemba **53**) na Hospitali za Wilaya **10** (Unguja **7** na Pemba **3**) zimeanzisha timu za kusimamia ubora wa viwango uanzishwaji wa timu hizi kutasaidia kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi.

**122. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara unazingatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia pamoja na mahitaji halisi ya Sekta ya Afya kwa wakati uliopo, Wizara imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya 2020-2025 na

kuandaa Mpango Mkakati wa Tano 2026-2030. Mpango mkakati huo utalenga kuimarisha utoaji wa huduma za afya, kuongeza ufanisi katika usimamizi wa sekta pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zinazokidhi mahitaji ya wananchi na malengo ya maendeleo ya Zanzibar.

**123. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na uimarishaji wa taarifa za afya kwa kufanya ufuatiliaji wa taarifa katika vituo vya afya. Ufuatiliaji huo umeonesha kuwa ukamilishaji wa ukusanyaji wa taarifa za huduma za afya umefika asilimia **91** na uwasilishaji wa taarifa kwa wakati umefikia asilimia **71**. Wizara inaendelea na mikakati ya kuhakikisha uwasilishaji wa taarifa kwa wakati unafikia asilimia **100** ili kuweza kufanya maamuzi sahihi ya kuimarisha huduma za afya.

**124. Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha huduma za Afya katika ngazi ya Msingi (Dispensari na Vituo vya Afya) zinaimarika, Wizara imeandaa Muongozo wa usimamizi wa matumizi ya fedha (Direct Health Facility Financing) unaolenga kupeleka rasilimali fedha ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya. Katika kutekeleza Muongozo huo, Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya **139** (Unguja **91** na Pemba **48**) zimeanzishwa na kupatiwa mafunzo ya muongozo huo ikiwemo kuandaa Mpango Kazi kwa kila Kituo. Aidha, Serikali kupitia Mfuko wa Huduma za Afya (ZHSF) inaviwezesha Vituo vya Afya kifedha ili kufikia huduma bora za afya kwa wote.

**TAASISI YA UTAFITI WA AFYA (ZAHRI)**

**125. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Afya ina jukumu la kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za afya Zanzibar kwa lengo la kuzalisha ushahidi wa kisayansi unaosaidia katika kupanga, kutekeleza na kuboresha huduma za afya pamoja na kusimamia maadili ya tafiti za afya na matumizi ya matokeo ya tafiti katika kufanya maamuzi.

**126. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Huduma hii ilikadiriwa kutumia **TZS. 2.47 bilioni** Ruzuku ambapo **TZS 1.78 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS. 0.69 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 1.49 bilioni** sawa na asilimia **80** ya makadirio ya Ruzuku ya miezi tisa ilipatikana ambapo **TZS 1.32 bilioni** Ruzuku ya Mishahara na **TZS. 0.17 bilioni** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo.

**127. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha tafiti moja ya "***Value Addition"*** inayolenga kuongeza thamani ya dawa za mitishamba zinazotumika kutibu pumu, shinikizo la juu ya damu na kisukari. Tafiti nane (**8)** zinaendelea kufanyika ambazo ni tafiti ya Absorbent, BREEDIME, ZAN-TOTO*,* Matumizi ya Huduma ya Bima ya Afya kwa kuzingatia Usawa, ***"Fair Choices on the Path to UHC"***, Kurekebisha na Kuingiza Programu ya Elimu ya Lishe katika Huduma za Utunzaji wa Afya ya mama mjamzito na DAWA PROJECT.

128. **Mheshimiwa Spika,** Kukamilika kwa tafiti hizo kutaiwezesha Wizara kufanya maamuzi sahihi ya kisera juu ya utoaji wa huduma za afya katika maeneo mbalimbali ya huduma ikiwemo kujua usugu wa dawa za antibiotiki kwa maradhi ya watoto na madhara yatokanayo na utoaji wa dawa usio sahihi kwa watoto pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali za sekta ya afya.

## M. PROGRAM NDOGO: URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA AFYA PEMBA (SH010303)

129. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipanga kutumia **TZS 31.84 bilioni** ikijumuisha **TZS 27.42 bilioni** kwa ajili ya mishahara na **TZS 4.42 bilioni** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 19.51 bilioni** sawa na asilimia **82** ya makadirio ya miezi tisa zimetumika. Fedha hizi zinajumuisha **TZS 18.91 bilioni** sawa na asilimia **92** ya makadirio ya miezi tisa zimepatikana kwa ajili ya mishahara na **TZS 0.60 bilioni** sawa na asilimia **18** kwa matumizi ya kawaida.

130. **Mheshimiwa Spika,** Wafanyakazi **610** walipewa likizo lao la kawaida, wafanyakazi **4** walichukuwa likizo bila malipo na wafanyakazi **4** walifariki dunia, Mwenyezi Mungu awajaalie malazi mema peponi, Amin.

131. **Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa uwepo wa chakula lishe katika vituo vya afya na hospitali za wilaya umefanyika kwa kushirikiana na maafisa lishe katika Timu za Afya za Wilaya.

Vituo **78** vya Afya na Hospitali tatu za Wilaya za Pemba zilifanyiwa ufuatiliaji wa uwepo wa chakula lishe. Aidha, vipindi kumi na moja (**11**) vya elimu vinavyohusu lishe vilirushwa (**6** TV na **5** Radio) ikiwemo radio jamii ya Mkoani na Micheweni. kwa upande mwengine Wizara kwa kushirikianana na Taasisi ya Lady Fatemah Trust Foundation watu **400** (Wanaume **175** na Wanawake **225**) walipatiwa elimu ya afya ya akili kwa Wilaya za Wete na Micheweni ili kupunguza athari ya matokeo yanayotokana na changamoto ya afya ya akili.

## N. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA AFYA

**Program Kuu: KINGA NA ELIMU YA AFYA**

**Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Afya ya Msingi;**

**132. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mradi huu ulitengewa jumla ya **TZS 20.00 bilioni** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, **TZS 10.81 bilioni** sawa na asilimia **72** ya makadirio kwa miezi tisa zimetumika kwa ajili ya malipo ya Vyeti *(Interim Payment Certificate)* mbalimbali za wakandarasi kwa vituo vya afya Sebleni, Tunguu, Mpendae, Rahaleo, Mahonda, Tumbatu, Welezo, Mtoni Basra, Nungwi kwa Unguja na kwa Pemba ni Kiungoni, Konde, Maziwa Ngombe, Jadida, Mtambile, Kiuyu Minungwini, Chonga na Kojani.

i. **Kumaliza Ujenzi wa Chomeo la Taka (Kibele na Vitongoji).**

133. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umepangiwa **TZS 2.00 bilioni** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2026 Wizara haijapokea fedha kwa upande wa Mradi huu. Aidha, **TZS 0.61 bilioni** zimepatikana kwa ajili ya kulipa deni kwa asilimia **28** la usambazaji, ufungaji wa Chomeo la Taka Unguja na Pemba. Mradi huu upo kwenye hatua za mkataba na kuanza kwa ujenzi.

ii. **Ujenzi wa Taasisi ya Afya ya Jamii - Binguni.**

134. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 2.00 bilioni**. Hadi kufikia Machi 2026 mradi huu upo kwenye hatua za mkataba kwa ajili ya kupata mshauri elekezi wa kuandaa michoro, makisio ya ujenzi na usimamizi wa ujenzi.

**Program Kuu: HUDUMA ZA TIBA**

**Program ndogo za Huduma za Matibabu**

iii. **Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mkoa.**

135. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 5.00 bilioni** kutoka Serikalini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi Hospitali za Wilaya Mbuzini na Hospitali ya Mkoa Mahonda na Ununuzi

wa Samani kwa nyumba za Wafanyakazi. Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 6.68 bilioni** sawa na asilimia **131** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana

**iv. Kuimarisha Miundombinu ya Afya**

- **Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa – Dunga Zuze - Unguja**

**136. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 7.00 bilioni** kutoka Serikalini. Mkandarasi tayari ameshapatikana na anasubiri malipo ya awali kuanza kazi.

- **Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja (Mahonda)**

**137. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 7.00 bilioni** kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026 mradi ulipangiwa kutumia **TZS 5.25 bilioni** Mkandarasi wa ujenzi "Cross World Contractors CO, LTD" anaendelea na hatua za awali za ujenzi (site settings).

- **Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba (Wete)**

**138. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 3.00 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 23.00 bilioni** kutoka kwa Washrika wa Maendeleo. Mradi huu unasimamiwa na Mshauri elekezi Octavo Solution

Private Limited. Mradi huu unajengwa na Mkandarasi Kampuni ya Abudhabi International Medical Services ambapo ameshakabidhiwa eneo la ujenzi ambapo mkandarasi atajenga jengo la litakalochukuwa vitanda 100. Aidha Serikali imepanga kuongeza jengo la ziada katika eneo hili litakalokua na idadi ya vitanda 100 ambalo litatoa huduma za kibingwa na bobezi. Hospitali hii inatarajiwa kuwa Hospitali ya mkoa wa Kaskazini Pemba. Mradi huu upo kwenye hatua za mkataba na kuanza taratibu za ujenzi.

- **Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kusini Pemba (Chake Chake)**

**139. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 2.90 bilioni** kutoka Serikalini. Mradi huu upo kwenye hatua za mkataba na kuanza taratibu za ujenzi.

- **Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Afya Pemba**

**140. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 2.50 bilioni** kutoka Serikalini. Hatua za kutayarisha michoro, makisio ya ujenzi zimekamilika. Hivyo ipo kwenye hatua ya kupata mkanadarsi wa ujenzi.

**v. Mradi wa ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja**

**141. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia **TZS 24.40 bilioni** (TZS **14.40**

**bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 10.00 bilioni** kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026 **TZS 4.62 bilioni** sawa na asilimia **76** zimepatikana ambapo **TZS 4.50 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 0.12 bilioni** kutoka kwa wahisani kwa ajili ya posho za wafanyakazi wa Usimamizi wa Mradi (PIU). Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, mradi huu umefanikiwa kukamilisha mchakato wa kumpata mkandarasi ambae ni China Jiaxi International Economic and Technical Co-Operational Engineering Company Limited. Aidha, kazi zinazoendelea kwa hatua za awali za ujenzi wa msingi na ujenzi umefikia asimilia **4** na utakamilika baada ya ya miezi **18.**

**vi. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali Rufaa na Kufundishia - Binguni**

**142. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia **TZS 17.56 bilioni** (**TZS 1.7 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 15.86 bilioni** kutoka Exim Bank ya Korea. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, **TZS 5.48 bilioni** zilipangwa kutumika **TZS 1.27 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 4.21 bilioni** kutoka kwa Exim Bank. Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 1.02 bilioni** sawa na asilimia **22** zimepatikana kutoka Serikalini kwa kazi ya Usimamzi wa Mradi. Serikali inaendelea na kusubiria hatua za Serikali ya Korea kumuidhinisha mshauri elekezi kwa ajili ya kuanza kazi.

**Program ndogo za Huduma za Uchunguzi (SH010202)**

**vii. Kuimarisha Miundombinu ya Afya**

- **Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu- Pemba**

**143. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 2.20 bilioni**. Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu itakayosaidia utoaji wa huduma katika udhibiti wa vyakula, dawa na vipodozi Zanzibar. Mradi huu umefanikiwa kufikia katika hatua za awali za uandaaji wa michoro.

- **Uanzishaji wa Kituo cha Kudhibiti Sumu na Kemikali Unguja**

**144. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 1.40 bilioni.** Hadi kufikia Machi 2026 hakuna fedha iliyotumika. Mradi huu unaendelea na hatua za maandalizi ya Michoro pamoja na Tathmini ya gharama (BOQ). Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu itakayosaidia utoaji wa huduma katika udhibiti wa sumu na kemikali Zanzibar.

- **Ujenzi wa Maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa- Pemba;**

**145. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 2.20 bilioni** fedha kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026 mradi huu

ulipangiwa kutumia **TZS 1.65 bilioni**. Hadi kufikia Machi 2026 Mradi huu umefanikiwa kumpata Mkandarasi wa Ujenzi hatua inayofuata ni kusainiwa kwa Mkataba wa Ujenzi.

- **Ujenzi wa Hospitali ya Makunduchi;**

146. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa **TZS 23.00 bilioni** ruzuku kutoka kwa Washirika wa maendeleo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, mradi ulipangiwa kutumia **TZS 17.25 bilioni**. Mradi huu unajengwa na Mkandarasi Kampuni ya CRJE ambapo kwa sasa ameshalipwa malipo ya awali **TZS 1.19 bilioni.** Mradi wa ujenzi unaendelea na upo katika hatua ya ujenzi wa msingi.

- **Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Saratani Binguni**

147. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia **TZS 0.80 bilioni** kutoka Serikalini. Mkandarasi amepatikana na kukabidhiwa eneo la ujenzi na sasa ameanza na hatua ya "site clearance" na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi wa Juni. Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na **AEGLE ONCO CARE CENTER LTD** kutoka Mauritius kupitia utaratibu wa EPCF+OT.

## O. PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)

### MAPATO

**148. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikadiriwa kukusanya **TZS 0.05 bilioni** kupitia vyanzo vya malipo ya Huduma za Afya, Huduma za Haraka (Fast Track), Huduma za Bima na malipo ya wanafunzi wa kigeni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 **TZS 0.04 bilioni** sawa na asilimia **89** zimekusanywa.

### MATUMZI

**149. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Hospitali ya Mnazi Mmoja Fungu (H02) imepangiwa kutumia **TZS 38.83 bilioni** kati ya hizo **TZS 22.81 bilioni** kwa ajili ya mishahara, **TZS 14.02 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa hospitali na **TZS 2.00 bilioni** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka Serikalini.

**150. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 18.78 bilioni** sawa na asilimia **64** ya miezi tisa ziliingizwa ambapo **TZS 14.99 bilioni** kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi na **TZS 3.00 bilioni** kwa uendeshaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja (HMM), Kidongo Chekundu na Mwembeladu.

**151. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Machi 2026, **TZS 0.79 bilioni** sawa na asilimia **53** ya miezi tisa zimeingizwa kwa ajili ya Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kutoka Serikalini.

**152. Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kupitia fungu **H02** ni kama ifuatavyo:

- Kuimarisha huduma ya uchunguzi wa matibabu ambapo vipimo vya maabara **77,438** na vipimo **7,462** kwa njia ya picha vilifanyika.
- Kuimarisha huduma za matibabu ambapo wagonjwa **42,318** (Wanaume **14,106** na Wanawake **28,212**) wamehudhuria katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kupatiwa huduma na matibabu. Aidha, wagonjwa **5,582** (Wanaume **3,465** na Wanawake **2,117**) wamehudhuria katika Hospitali ya Kidongo Chekundu na kupatiwa huduma na matibabu.

**153. Mheshimiwa Spika,** Wagonjwa **2,137** (Wanaume **486** na Wanawake **1,651**), walilazwa kwa magonjwa mbalimbali. Kwa upande wa Hospitali ya Kidongo Chekundu Wagonjwa **945** (Wanaume **556** na Wanawake **389**) walilazwa kwa matatizo ya afya ya akili.

**154. Mheshimiwa Spika,** Wajawazito **1,269** (Hospitali ya Mnazi Mmoja **754** na Hospitali ya Mwembeladu **515**) wamepokelewa, kati ya hao **276** wamejifungua kwa njia ya kawaida na **362** wamejifunguwa kwa njia ya upasuaji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wajawazito **515** wamejifungua katika Hospitali ya Mwembeladu kwa njia ya kawaida na wazazi **41** walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa uangalizi zaidi. Aidha, wajawazito **5** na watoto **22** walifariki dunia katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

155. **Mheshimiwa Spika,** Kambi **6** za kibingwa na kibobezi za uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa ikiwemo kambi **3** za upasuaji wa mgongo na ubongo, Kambi **2** za macho na kambi **1** ya kina mama kwa mashirikiano na madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja na wataalamu kutoka Hospital ya Taifa ya Muhimbili, Spain na Norway. Jumla ya wagonjwa **662** (wanaume 188 wanawake 474) walichunguzwa na kupatiwa matibabu. Kati ya hao wagonjwa **210** (wanaume 89 na wanawake 121) wamefanyiwa upasuaji.

## P. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

156. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepitia changamoto zifuatazo: -

i. Msongamano mkubwa wa wagonjwa kutokana na uhaba wa watumishi na wananchi kutofuata mfumo wa rufaa;

ii. Kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) na ajali za barabarani;

iii. Uhaba wa madaktari na wauguzi bingwa na bobezi na huduma nyengine za kitaalamu; na

iv. Upatikanaji wa fedha usioridhisha kwa ajili ya uendeshaji wa wizara na miradi ya maendeleo.

## Q. HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO

**157. Mheshimiwa Spika;** Kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji majukumu hayo, Wizara imejipanga kutatua kama ifuatavyo: -

i. Kajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Raisi, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulingana na mahitaji;

ii. Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kufuata taratibu za rufaa na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya Unguja na Pemba;

iii. Kuongeza uhamasishaji wa elimu ya afya kwa jamii dhidi ya maradhi yasioambukiza (NCDs), pamoja na ajali za barabarani kwa kushirikiana na wadau wengine. Vile vile hatua za awali za ujenzi wa Hospitali ya kisasa ya maradhi ya saratani zimeshaanza ambapo ujenzi huo unatakiwa kuaza mwezi Juni 2026.

iv. Kusomesha wataalamu bingwa na bobezi kwa kupitia programu maalum za vyuo vya Jumuiya ya Afya za nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (ECSA-HC), ambapo mafunzo hayo hufanyika katika Hospitali zetu 10 za Wilaya na 2 za Mkoa. Mafunzo haya yanasaidia kupunguza kwa haraka uhaba wa wataalamu kwa kuwabakiza kwenye vituo vyao vya kazi huku wakiendelea na masomo yao; na

v. Kuendelea kusomesha wataalamu bingwa na bobezi katika fani zenye uhaba wa huduma za kibingwa na bobezi.

## R. MUELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/ 2027

158. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 naomba sasa niwasilishe vipaumbele vya Wizara ya Afya na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2026/2027.

159. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Afya itaanza kutekeleza Mkakati wa **V** wa Sekta ya Afya kwa kuzingatia mihimili mikuu sita **(6)** ya Sekta ya Afya ambayo itazingatia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

### I. KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA

i. Kuimarisha Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto;

ii. Kuimarisha huduma za Afya ya Msingi (PHC) na Afya ya Jamii;

iii. Kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza;

iv. Kutekeleza mpango mkakati wa kisekta wa lishe wa mwaka 2024/2025 – 2028/2029;

v. Kuimarisha huduma za msingi za afya ya akili; na

vi. Kuwekeza katika malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kuanzia umri 0 mpaka miaka 8.

## II. KUIMARISHA NGUVU KAZI KATIKA SEKTA YA AFYA KWA NGAZI ZOTE

i. Kuajiri na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya;

ii. Kupanua wigo wa programu za mafunzo ya kujiendeleza kwa wauguzi, wakunga, na wataalamu wa kada nyengine za afya;

iii. Kuimarisha mfumo wa kidigitali wa kuhifadhi kumbukumbu za taarifa za wafanyakazi; na

iv. Kuimarisha mazingira ya kazi, motisha, na maendeleo ya kazi ili kupunguza uhamaji wa wafanyakazi.

## III. KUIMARISHA UGHARAMIAJI ENDELEVU WA HUDUMA ZA AFYA

i. Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kugharamia Huduma za afya;

ii. Kushajihisha sekta isiyo rasmi kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya; na

iii. Kushajihisha sekta binafsi katika uwekezaji na utoaji wa huduma za afya.

